

UKAMILIFU

 Asante, Ndugu Neville. Habari za asubuhi, marafiki. Nina furaha kurudi asubuhi ya leo, nami naweza kutoa tamshi lile lile juu ya ndugu yetu. Nilikuwa nimemwahidi nitakuwa kwenye matangazo ya redio, nami nikachelewa kwa juma moja, halafu juma lililofuata nikasahau jambo hilo. Kwa hiyo nikafikiri mara ya tatu unapaswa kuwa wa—wakati mzuri sana, inapaswa kufanywa hivyo.

² Kwa hiyo nilikuwepo tu kule, katika dakika moja ya wakati, dakika moja tu. Naye Ndugu Snyder alikuwa nje, kwa hiyo tuliingia kisirisiri upesi sana, na—na hatimaye tukaingia kwenye matangazo. Nami nafikiri tuliwasumbua, ndivyo tulivyofanya, tulipoingia namna hiyo, kidogo tu. Kwa hiyo . . .

³ Nami huyu hapa, naja, nilifikiria juu ya somo la kuhubiri, mwajua. Na kwa kawaida yangu, inachukua kama saa moja na nusu. Nami nilipata kama dakika kumi na tano, kumi na nane za kuanza, ndipo nikaangalia juu, nayo saa ikasema wakati wa kuondoka umewadia. Kwa hiyo tutaendelea Jumamosi ijayo, ama wakati fulani. Sawa.

⁴ Jumapili iliyopita, tulikuwa kwenye sura ya 10 ya Waebrania, na tukalianza kwenye aya ya 1, wala hatukuendelea mbali zaidi.

⁵ Msisahau zile ibada huko Indianapolis juma hili. Kama ye yote wenu, ama mna marafiki wote kule, mbona, waandikieni na muwaarifu. Ibada zitaanza kesho usiku kwenye saa moja, kwenye Maskani ya Cadle huko Indianapolis. Na kuna nafasi nyingi za kuketi, karibu watu elfu kumi na moja wata—wataketi. Na ni mkutano mdogo, ni—ni shirika dogo. Hata kweli sijui jina la shirika hilo. Wao wana m—mkutano wa kambi kule, ama mkutano.

⁶ Na katika mkutano huu wao waliniomba nihubiri usiku. Kwa hiyo ule . . . Nafikiri ushirika huo wenyewe, kanisa hilo, shirika hilo lina watu wachache, wachache sana. Na kwa hiyo . . . Na basi, usiku, nina ninii—ninahubiri kwenye ibada kila usiku, Jumatatu mpaka Ijumaa. Ijumaa jioni ndio mwisho wa mkutano huo. Kwa hiyo, kama mna marafiki wote karibu na Indianapolis, mbona, mnakaribishwa.

⁷ Halafu tarehe ishirini na tatu, asubuhi ya tarehe ishirini na tatu, kama ikitokea kuna mtu anayepitia hapa, kwenye likizo yako; kwa kuwa ni mwezi wa likizo, kwa kawaida, Juni. Minneapolis, Wafanyi Biashara Wakristo Kimataifa watakuwa na mkutano wao Minneapolis. Na ibada ya watu wote ni ya tarehe ishirini na tatu, kifunguakinywa. Kifunguakinywa

cha asubuhi ni cha tarehe ishirini na tatu Juni. Ninatazamia kuhubiri kwenye kifunguakinywa cha asubuhi, kufungua ibada.

⁸ Halafu, tarehe ishirini na nne, nitakuwa ningali Minneapolis, nami nitakuwa kwenye Maskani ya Heart's Harbor, pamoja na Kasisi Gordon Peterson. Nao wataanza kipindi hicho kwa redio huko. Kwa hiyo kama mko—mko karibu, mbona, manakaribishwa.

⁹ Halafu kwenye tarehe ishirini na nne, ama ishirini na tano, hasa, mkutano unaanza, nasi tutakuwa pale. Ni mpango usio wa kawaida sana. Bw. Roberts, Bw. Hicks, mimi mwenyewe, wahudumu wengi zaidi, watakuwapo pale. Na hakuna utaratibu uliowekwa. Wafanyi Biashara Wakristo, kwa kuwa wao ni Wafanyi Biashara Wakristo wa Injili Yote, walitaka kuuacha wazi, kwa yo yote Roho Mtakatifu angesema kifanywe; watuweke sisi sote pale. Nao hawajakuwa na mmoja kama huo, wala hawakutangaza wahubiri wo wote. Tangazo pekee la mahubiri—mahubiri yaliyotangazwa ni—ni asubuhi ya tarehe ishirini na tatu. Ninatazamia kuhubiri kwenye kifunguakinywa chao, na hilo limetangazwa. Ama kweli, sote tutakuwa kule, tukimngojea Roho Mtakatifu. Hilo linapaswa kuwa ni jambo zuri sana, siyo? Kama sote tunaweza tu kujitoa kwa Roho Mtakatifu, ndio sawa, tumwache Yeye atutumie jinsi—jinsi angetaka kututumia, sasa.

¹⁰ Halafu mkutano mwingine uliopangwa, ambao nina habari zake, ule Mkutano wa Barabara ya zamani ya Azusa. Ni... Huo unakuja tarehe kumi na tano Septemba. Nitafungua ibada kule kwa ajili ya mkutano wa kimataifa wa Barabara ya Azusa; miaka hamsini ya pentekoste katika Marekani. Wao wana umri wa miaka hamsini, Septemba hii ijayo, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka kwa mara ya kwanza huko kwenye Misheni ya Barabara ya Azusa. Ile ya kale... ninaamini ilikuwa ni misheni ya kale ya Kibatisti, ama Barabara ya Azusa huko Los Angeles, California, ndiko ambako Roho Mtakatifu alishuka kwa mara ya kwanza, miaka hamsini iliyopita, Septemba hii ijayo.

¹¹ Na wakati nilipokuwa kwenye Cow Palace, miaka michache iliyopita, nilisema... Vema, hamsini, neno *pentekoste* maana yake ni "hamsini," kwa hiyo mbona tusiwe na mkutano mkubwa. Na, wajua, hilo lilipamba moto, na wamepanga mkutano mkubwa wa kimataifa. Nao utafanywa katika Hekalu la Angeles. Na siku tano kabla ya huo, nitafanya safari ndogo ndogo kando ya kutembelea mahali mbalimbali. Loo, kule chini kwenye East Gate na... ama ninamaanisha South Gate, na kuendelea mpaka kwenye lile—lile jiji la... Loo, miji kadha hiyo midogo, miji mitano mbalimbali, kufanya safari fupi, ibada ya usiku mmoja, kisha niende moja kwa moja kwenye—kwenye huo mkutano mkubwa.

¹² Na kama mko karibu na California, ama huko nje, baadhi yenu mnaotoka California, kumbukeni jambo hilo. Tunatarajia wakati mzuri sana wa ushirika pamoja na watu wa Mungu kwenye wakati huo.

Sasa na tuombe.

¹³ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru, asubuhi ya leo, kwa sababu ya majaliwa makubwa na yenye utukufu tuliyo nayo ya kuja kwenye Uwepo Wako, kwa mioyo yenye furaha na shukrani, kwa kuwa Yesu Mwana wa Mungu ameturuhusu hivyo kufanya jambo hili. Na neema yake imetufikisha wakati huu. Nasi tuna furaha kuwa hapa leo.

¹⁴ Tunafurahi kupapapata mahali hapa padogo pa kukutania. Ni mahali palipo wazi, Biblia wazi, mioyo wazi, kulipokea Neno la Mungu na Ujumbe Wake. Nasi tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atakuja na kujaza kila mwanya wa moyo wetu kwa wema Wake, tunapolisoma Neno Lake. Kwa maana imeandikwa, “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Kwa hiyo, Ee Mungu, fungua kinywa chetu leo, ili kwamba iwe ni Wewe unayenena, na mioyo yetu, ili kwamba iwe ni Roho Mtakatifu anayesikia. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

¹⁵ Jumapili iliyopita, katika Kitabu cha Waebrania, tulianza na sura ya 10, ndipo tukaingilia somo lingine, bila kujua ni wapi Roho Mtakatifu atakakotuelekeza ku—kufundisha, hakuna kitu kilichotangulia kupangwa, ni kungojea tu kutenda Kwake. Tulifikia kwenye kutangulia kujua, kutoka kwenye jambo hilo.

¹⁶ Aisee, jambo lingine, nina furaha kumwona Dada Hooper ameketi pale, asubuhi ya leo. Dada Flo, hakika nina furaha kukuona. Wengi wenu huenda msimjue, wengine wenu. Naye ameugua kifua kikuu kwa miaka kadha wa kadha, na hawezi kitandani, na kila mahali nchini, akijaribu kupata ukombozi. Na, leo hii, tunafurahia kuwa naye ameketi maskanini, akionekana mzima, leo. Mungu ashukuriwe!

¹⁷ Sasa, mwandishi wa Waraka wa Waebrania anadhaniwa kuwa ni Paulo, kwa maana inasikika kama kwamba ni maandiko yake. Nao Waraka wa Waebrania ulikuwa kwa ajili ya Wayahudi, Waebrania. Na ilikuwa ni Paulo akijaribu kutenganisha torati na neema, akionyesha to—tofauti kati ya sheria ilikuwa ni nini, na neema ni nini, kwa maana Waebrania walikuwa chini ya torati. Na basi Paulo alikuwa akijaribu kuwaonyesha neema ilikuwa ni nini. Nami nafikiri, mimi mwenyewe, ya kwamba sura ya 10 hapa, na aya ya 1, ingekuwa ufunguo mkamilifu kwa jambo hilo lote.

¹⁸ Sasa tuna sura ya 1, ikianza hivi. “Mungu, kwa sehemu nyingi, kwa njia nyingi alisema zamani na baba zetu katika manabii, lakini katika siku hii ya mwisho amesema na sisi katika Mwanawe, Kristo Yesu.”

- 19 Fungueni sura ya 7, kule kutokea kwa “Melkizedeki.”
- 20 Tunashuka kuja kwenye sura ya 9, ya “ukuhani,” jinsi ambavyo Kristo anakuwa Kuhani wetu Mkuu, kupachukua mahali pa yule kuhani mkuu wa kale.
- 21 Kisha tunalileta kwenye sura ya 10, tunaingia, “Kwa kuwa torati ni kivuli cha mema yatakayokuja.”
- 22 Tunaingia kwenye sura ya 11, na yote ni juu ya vile—vile vivuli vizuri sana vya imani, wale watu mashujaa wa imani, jinsi “kwa imani” walifanya jambo *kadha na kadha*. Na jinsi, “Pasipo sisi wao wasingeweza kukamilishwa, kwa kuwa wao ni kivuli cha hawa wajao.” Halafu tunaingia katika sura ya 11, naye Paulo . . .
- 23 Ama, sura ya 12, Paulo akisema, “Kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu.”
- 24 Sura ya 13, sura ya mwisho, ilisema, inaishia hapa, kuelekea mwisho, ya kwamba Yesu Kristo ni yote katika yote, ya kwamba, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Mnaona? Ikionyesha ya kwamba ilikuwa ni Kristo kule nyuma kabla ya torati, ilikuwa ni Kristo katika torati, ilikuwa ni Kristo katika siku za neema, itakuwa ni Kristo milele. “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ni picha nzuri namna gani ambayo Waraka wa Waebrania unatuchorea.
- 25 Sasa, tukianza sasa tena na aya ya 1, hebu turudi nyuma. Jumapili iliyopita, tulifikiri tungefikia kwenye somo la *ukamilifu*, lakini basi Mungu akaturudisha nyuma na tukachukua *kujua tangu zamani*, akituonyesha ambapo kabla ulimwengu haujafanywa. . . Ni wangapi waliokuwa hapa Jumapili iliyopita? Hebu tuone mkono wako. Mlipata jambo hilo? Kabla ulimwengu haujafanywa, tuliwekwa katika Kristo. Wazia jambo hilo.
- 26 Mungu, akiwa asiye na mpaka, Ambaye hawezi kusema uongo, hawezi kusema kitu kilicho kinyume, anajua kila kitu, ni mkamilifu tu hapo mwanzo kama alivyo wakati wa mwisho, na ni mkamilifu tu mwishoni kama alivyokuwa hapo mwanzo. Mungu hana mpaka, kama vile Milele. Usingeweza kupata kona ya duara kamilifu. Unaweza kukimbia na kukimbia kwenye miaka, na Milele, na kamwe, kamwe, kamwe kusingeweza kuwa na mwisho wake. Na hivyo ndivyo jinsi alivyo Mungu. Na wakati Yeye ni wa kwanza, alikuwa . . . Mungu, aliyekuweko daima, alikuwa hana kikomo, mkamilifu, kwanza, Naye daima atakuwa yeye yule. Hawezi kubadilika kamwe. Yeye ni mkamilifu vile vile.
- 27 Sasa mnyororo huu mkuu wa ukamilifu ulivunjwa na majira ya wakati. Wakati ulikuja, kwa sababu ya dhambi. Hebu tuchore picha ya wakati. Hebu tuone duara kamilifu, milele,

milele. Na basi, mara, dhambi ikaingia, na kuweka ninii—ninii ndogo... Kama mke wangu anavyoiita, “kovu” dogo, ama tone dogo kwenye mnyororo. Kwa hiyo, inashuka chini sasa. Milele inaendelea, bali haiko katika hali yake kamilifu. Hili hapa pengo dogo linaloshuka, linavunja upande *huu*, linatokea upande *huu*. Ilimbidi Mungu kufanya jambo hilo kwa sababu Shetani alisababisha jambo hilo. Nayo ikashuka ikaingia katika muda wa wakati, kwa ajili ya kujaribiwa, na kukamilishwa, na kwa kuwatakasa waliopotoea. Kwamba, Mungu kwa neema yake ya mamlaka Yake, huenda siku moja ikainua kovu hilo dogo, ama pengo, na kulirudisha kwenye duara kamilifu, ndipo itavingirika namna ile ile. Mnaona jambo hilo?

²⁸ Wakati! Sasa, wakati ndio duara hili dogo; inashuka na kufanya duara. Yesu alikuwa tangu Milele hata Milele, bali aliingia katika muda wa wakati na kufanyika mwili, kisha akapitia hapa kusudi apate kutakasa, ama kuweka mlia wa Damu mahali hapa, ili kupakomboa na kupashikamanisha na Mungu tena, kwa Milele yote. Mnaona jambo hilo? Hivyo tu ndivyo wakati ulivyo.

²⁹ Halafu, Mungu, wakati ilipoanza hapa, katika mwisho wa ile dosari kwenye hiyo duara kamilifu, hiyo ilisababisha dosari ndogo ndani yake. Wakati Mungu alipoanza kule, Yeye alikuwa mkamilifu. Kila kitu alichosema kilikuwa kikamilifu. Kila kitu alichofanya, anachofanya, ni kikamilifu.

³⁰ Kwa hiyo, basi, Biblia ilisema, ya kwamba, “Kristo Yesu alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu,” mwanzo wa ile dosari ndogo, “kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Kristo aliuawa hapo mwanzo. Sasa, Yeye kwa uhalisi hakuuawa mpaka miaka elfu nne baadaye. Lakini, sababu ya Yeye kuuawa wakati huo, kwa sababu, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.” Unaona, Ndugu Egan, ninalomaanisha? Unaona? Yeye alikuwa Mungu, hapo mwanzo. Na wakati...

³¹ Sasa, Shetani angeweza kuninii... haku—hakuumba duara hili dogo, kovu hili dogo. Yeye hakuliumba hilo. Shetani hawezi kuumba. Shetani anaweza tu kupotosha kile Mungu ameumba.

³² Angalia, ninasema jambo hili kusudi mfahamu. Hili ni darasa la watu wazima, na karibu sisi sote ni watu waliooa, labda asilimia tisini. Nami natumaini vijana wanawake na wanaume wanafahamu sauti yao, kile mimi... Mnanifahamu mimi, kuelezea tu jambo fulani.

³³ Kama mwanamume akijitwalia mke, mwanamke, naye anakuwa mkewe, nao wanaishi pamoja kama mume na mke kwa miaka hamsini; wao ni wasafi tu na weupe na wasioghoshiwa kana kwamba hawakujuana kimwili kamwe. Huo, huo ndio mpango wa Mungu. Lakini kwa mwanamume huyo ama mwanamke kwenda na kuishi na mwanamume mwingine ama

mwanamke, jambo hilo hupotosha, linasababisha kuzaliwa kwa watoto haramu. Lakini kama wakiishi pamoja katika upatano huo mkamilifu, hiyo ndiyo njia ya Mungu. Lakini Shetani huja na kutia tamaa ndani ya mwanamume huyo ama mwanamke, nao wanaishi kinyume cha nadhiri zao za ndoa, na huko ni kupotosha. Ni kujuaana kimwili kule kule, lakini kumepotoshwa.

34 Kwa hiyo hivyo ndivyo Shetani afanyavyo na kitu halisi cha Mungu, yeye hukipotosha. Hivyo ndivyo Shetani anavyofanya leo na watu walio halisi, na wa kweli. Sikilizeni. Ujumbe halisi wa Mungu, yeye huupotosha, anaufanya jambo lingine, anaufanya uonekane kuwa ni kitu usicho.

35 Ulimwenguni siku hizi, tunaona ya kwamba kuna watu, Biblia inabashiri jambo hilo, tabaka tatu za watu.

36 Moja ni ya baridi, gumu, ya kawaida, isiyojali, nao wanaendelea tu, si zaidi ya kuwa kwenye loji. Wao huenda kanisani, wanazungumza kidogo juu ya *hiki, kile*, na juu ya Bwana, na kadhalika, wanarudi, bali hawana ujuzi halisi wa kuzaliwa mara ya pili. Loo, wengine wao wanadai jambo hilo, bali maisha yao yanathibitisha ya kwamba sivyo ilivyo. Sasa, hilo ni kwa upande mmoja, kule mbali sana.

37 Na sasa, hapa chini upande wa pili, washupavu wa dini, na kanisa halisi na la kweli, Yesu alisema jambo hilo, “Wangefanana sana, ingewapoteza walio wateule.”

38 Sasa, watu wengi, mara waonapo ushupavu wa dini umechanganyikana na walio wa kweli, “A-ha,” wao wanasema, “hakuna lo lote Kwake,” wanaendelea. Mnaona, hilo ni jambo lile lile Mafarisayo walilofanya. Shetani, hajipumbazi kwa kujaribu kupotosha hao. Yeye anajaribu kupotosha Kweli hii. Na huyu mshupavu wa dini hapa anajaribu kuigiza Kweli ile. Mnaona? Hapo ndipo mstari wako wa hatari ulipo, papo hapo.

39 Sasa, inatupasa kudumu wa kiroho, kusoma Neno. Na jambo lo lote likizuka, nje, kinyume cha Neno, basi litupilie mbali. Hiyo ndiyo sababu, mara nyingi, ya kwamba nina- . . .

40 Wao wanasema mimi ni mkali sana kwa wahubiri wanawake. Biblia inasema wasiseme kanisani. Biblia inawakataza kunena kwa lugha, ama cho chote kile, kanisani. Sina budi kudumu na Neno, kuliangalia mahali lilipo, kuliangalia.

41 Katika ulimwengu siku hizi, ambamo itikadi hizi zote zinainuka, angalia, kwenye madhehebu yote ya kutokula nyama. Na washika sheria, ya kwamba, “Inanibidi kufanya *hivi na vile*. “Kama sineni kwa lugha, kama sifanyi jambo *hili*, kama sipazi sauti, kama sichezi, nina kasoro.” Huko ni kuishi kwa sheria.

42 “Tumeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani.” Si yale umefanya; ni yale aliyofanya Yeye. Yeye alifanya ambayo usingeweza kufanya. Kama ungaliweza kujiokoa mwenyewe,

basi isingalimpasa Yeye kufa. Bali Yeye alikufa, kusudi akuokoe, ambapo usingeweza kujiokoa.

⁴³ Ile methali ya kale ya kutomcha Mungu, inasema, “Mungu huwasaidia wale wasioweza kujisaidia...” Ama, “Mungu husaidia hao wanaojisaidia,” wao husema. Hiyo ni vinginevyo tu. Kama unaweza kujisaidia, Mungu anakutarajia kujisaidia. Mungu huwasaidia hao wasioweza kujisaidia. Nawe huwezi kujisaidia, kuokolewa, kwa hiyo Mungu, kwa neema Yake, alikuokoa.

⁴⁴ Sasa, angalieni jinsi lilivyo jambo zuri. Torati, iliyo kuu katika Umilele, jinsi Mungu alivyotangulia kuiona duara hii. Na iwapo Yeye hana mwisho, wala hawezi—hawezi kuwa kitu kingine. Hebu nichukue tu jambo hili, kama dakika tano, kusisitiza jambo hili, kulikaza, kulipigilia, ili lisije likaponyoka likatoka kamwe niani mwenu tena. Roho Mtakatifu na aje aliunganishe pamoja na upendo, kusudi msiliache kamwe.

⁴⁵ Sasa angalia. Mungu, Ambaye hawezi kusema uongo; Mungu, Ambaye hana kikomo. Nami nasema jambo hili tena kwa ajili ya watu ambao inaonekana hawawezi kuvutiwa na kuponya Kiungu. Kama Mungu aliahidi jambo hilo, Mungu hana budi kushughulikia ahadi Yake. Hawezi kuiacha.

⁴⁶ Sasa angalia. Kabla Yeye hajaweka Neno lililoandikwa, na, *Hili* ndilo nia ya Mungu. Hili hapa. Hii ndiyo nia ya Mungu, ambayo Yeye aliwazia, kabla misingi ya ulimwengu haijapata kuwekwa. Ndivyo lilivyo. Hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kuiweka kwenye Neno lililoandikwa, na kusema mambo yatakayotokea, kwa maana Yeye aliona jambo hilo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na alijua jinsi tu jambo hilo lingekuwa, kisha akalinena.

⁴⁷ Kisha akawapa manabii maarifa Yake, nao wakayaandika. Na mwaka baada ya mwaka, na karne baada ya karne, tunalionika likitimia vile vile hasa. Mungu, akitoa kivuli cha lile la Kale, kuwa mfano wa lile Jipya. Nasi tunalionika Hilo, Neno kwa Neno, likitimizwa. Ni imani jinsi gani inayotubidi kuwa tumeimarisha katika Mungu!

⁴⁸ Sasa mwangalie Yeye, “Kristo akiuawa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

⁴⁹ Wakati Mungu alipotazama chini na kuona kitu pekee ambacho kingeweza kumwokoia mtu aliyepotea, Yeye alisema... Sijui kama haya ndiyo maneno yale, bali ilikuwa kitu kama hiki. “Mwanadamu hawezi kuokolewa, kwa maana atafanya dhambi. Bali ninaangalia kila mahali kule chini na kuona makumi elfu ya mioyo miaminifu itakayokuja. Ninaona maelfu ya watu ambao watataka kuokolewa, na wasitake kuingia kwenye maangamizi haya ya kutisha yatakayonibidi kumtengenezea Ibilisi na malaika zake, kwa maana hawana budi kuingia katika adhabu ya milele. Na watu wenye mioyo miaminifu wataona

jambo hilo. Nami nita—nitakuwa na mtu jina lake Esau azaliwe; kutakuweko na mmoja, Yakobo. Naye Yakobo hatakuwa mzuri sana, kwanza, lakini katika moyo wake atapenda mambo ya Mungu, kwa hiyo nitamchagua Yakobo.”

⁵⁰ Yeye alikuona wewe na akajua ya kwamba ulitaka kuokolewa. Kwa hiyo akasema, “Jambo pekee ninaloweza kufanya ni kushuka niende, Mimi Mwenyewe, na kuwa na Mwana azaliwe, ama mwili wa nyama, na kufanyika kama wao.” Tiba ni Mungu Mwenyewe afanyike dhambi, kusudi apate kulipia gharama. Kwa sababu, inatakiwa kitu cha hali ya juu sana kilichopo, kumwinua mwanadamu kutoka katika hali ya kupotea.

⁵¹ Basi, angalia, Yeye yuko juu ya kila Malaika, kila Malaika Mkuu. Aliye wa hali ya juu sana aliyekuwako, alishuka akaja duniani, akaishi kati ya wanadamu. Kisha akaenda kwenye mji ulio chini sana duniani, Yeriko. Naye alikuwa duni sana, hata mtu aliye mdogo sana mjini ilimbidi kuangalia chini apate kumwona Yeye; Zakayo. Halafu, basi, akafa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu. Akaja kupitia kwenye hori la ng’ombe, maskini. Aliye tajiri sana... Loo, natumaini mnafahamu jambo hilo. Aliye tajiri sana akawa maskini kuliko wote.

⁵² Hata katika usiku wenye dhoruba, alisema, “Ndege wana viota, na mbweha wana mapango, lakini sina hata pa kulaza kichwa Changu.” Aliye wa hali ya juu sana katika mbingu zote za Mbingu, akafanyika aliye wa chini sana kuliko wote. Hata jamii ya wanyama, walikuwa na majaliwa, Kwake, zaidi Yake, kulingana na faraja ya maisha.

⁵³ Si hayo tu, bali, katika kifo Chake, alikufa kifo ambacho hakuna mtu aliyepata kufa; kamwe, katika wanadamu, hapajakuwa mtu aliyepata kuvunjika moyo namna hiyo mpaka Damu Yake na maji vikatengana kabla hajafa.

⁵⁴ Aliye maskini kuliko wote; kutoka aliyetajiri kuliko wote, akawa maskini kuliko wote. Kutoka aliyebarikiwa kuliko wote, akawa mwenye kuteseka vibaya sana kuliko wote. Halafu, mbali na hayo, akashuka akaenda kwenye vilindi vya chini sana vya kuzimu iliyo chini sana, akiichukua dhambi yetu. Ndipo akaichukua ile ncha ya ule uzi, ama ncha ya ile kamba, kutoka kwenye ile dosari. Pale, akaiinua katika ufufuo, na kuiunganisha na sehemu ile nyingine ya Milele, na kufanya Barabara Kuu ya utakatifu, kusudi wasio safi waweze kuja na kusafiwa.

Kupitia kwenye kijito kilichojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye vena ya Imanueli,
Wenye dhambi wanapojitumbukiza chini ya
hayo mafuriko
Hupoteza waa lao la hatia.

⁵⁵ Njoni kwenye Barabara Kuu kuu. Na siku moja, Yeye Yule aliyekuwa kwenye mwanzo wa siku, atasimama kama mzee wa

siku, naye ataivuta ile kamba kuu ya Injili. Na wote walio kwenye Barabara hiyo Kuu, tangu mwanzo wa siku, mpaka zamani za kale, hata mwisho wa siku, watainuliwa; huku anapouondolea mbali wakati, kuingia katika Umilele. Mnaona jambo hilo? Huyu hapo, “Mtawala pekee aliye wa kweli; Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana.”

⁵⁶ Yeye alifanyaje jambo hilo? Kwa kutangulia kujua. Yeye alijua. Ndipo akasema, ya kwamba, “Yeye alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa.” Halafu, kama Yeye alikuwa hivyo, miaka eltu nne baadaye ikatimia, wakati ukaisha. Yeye akazaliwa, wakamfanya yale Yeye alisema wangemfanyia, ndipo akasulubishwa na kuuawa. Lakini, kweli, “Yeye aliuawa kabla ulimwengu haujaanza,” kwa maana Mungu alitangulia kumwona Yeye na kusema jambo ambalo lingetukia. Na wakati Mungu anaponena, haina budi kutimia. Mnaelewa? Loo, jamani! Mungu alitangulia kumwona Kristo, na haina budi kutimia. Hiyo ndiyo sababu ilikuwa tayari imekwisha. Wakati Mungu aliponena Neno, hiyo ilikwisha. Hiyo ndiyo sababu alikuwa kweli ametangulia kuonyesha kwa mfano, akauawa, wakati Mungu aliponena Neno kabla ya ulimwengu.

⁵⁷ Angalia! Si kwamba tu Kristo aliuawa, kuziondoa dhambi, bali jina lako liliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu aliandika jina lako, akalishirikisha pamoja na Lake, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

⁵⁸ Sasa, Shetani, anawafanya waogope sasa, anawafanya washuku jambo hilo?

⁵⁹ “Kabla ulimwengu haujaanza bado, Mungu aliita jina lako, ninyi Wakristo, na kuliandika katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ulimwengu haujaanza,” inasema Biblia. Hilo ni Neno la Mungu, Yeye alilinena kule nyuma, na kulifunua kupitia watumishi Wake, manabii, nasi tunafurahia baraka za kustarehe, na kukungojea kule Kuja kwa Bwana. Tunangojea, kwa subira. Yote imekwisha. Loo!

⁶⁰ Si ajabu, maradhi, hatari, mauti, hakuna kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo! Kwa sababu, kuwekwa misingi ya ulimwengu... Yeye alituweka kwenye Barabara hiyo Kuu ya kale yenye fahari, akapanda kwenye upindi wa mvua unaolala sawasawa, akaingia kwenye upeo wa mwanzo wa siku tena, huku anashika zile kamba mikononi Mwake. Na siku moja, atasema, “Njoni huku!” Sisi tulio hai na tuliosalia hata Kuja kwa Bwana, hatutawatangulia hao waliokwisha kufa kwenye Barabara Kuu, kwa kuwa parapanda ya Mungu italia nao waliokufa katika Kristo watafufuka. Nasi tutanyakuliwa pamoja, kuwalaki, huku ule mnyororo ukiinuliwa na kurudishwa kwenye ile duara ya Milele. Ndipo nyakati zikiendelea, sifa Zake tutaimba.

⁶¹ Yeye anafanya nini? Kule juu, akitujengea makao. “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao Mengi; kama sivyo, ningaliwaambia. Nami nimeshuka nikaja huku, bali nitaenda kuwaandalia moja, niyatayarisha yote. Na kama nikienda, nitarudi tena, kuwapokea Kwangu.” Loo, jamani! Naye anatuandalia mahali.

⁶² Wakati mwili huu mchafu unaopatikana na mauti, ulio hapa duniani, utakuwa...tutatenganishwa nao, utatupwa nje ya mnyororo wa Milele. Utakuwa nje ya shimo kubwa, ambalo hakuna mtu anayeweza kulivuka, ama aliyeweza, ama atakayeweza kamwe. Na wakati kiungo hiki hapa chini, kimeinuliwa hata kwenye sehemu ile, ambayo ni Barabara Kuu takatifu na iliyosakifiwa, ambayo Mungu alisema, hapo mwanzo, “ambako hakukuweco na kitu cha kutia unajisi; hakuna kitu cha kuangamiza.” Nayo dhambi ilisababisha duara hii. Ndipo wakati duara hii inapoendelezwa, moja kwa moja kupitia hapa kuwaleta wajumbe, na wakati itakapovutwa pamoja, kukutana na kila mwisho, Milele itaendelea. Wale waliokombolewa watatembea mle. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Loo, laiti ningaliweza kuimba. Ningetaka kuimba ule wimbo wa kale.

Kuna maskani nzuri huko mbali ng'ambo ya bahari,

Kuna makao yaliyobarikiwa kwa ajili yako na yangu!

Minara inayometameta, jua...itang'aa zaidi ya jua,

Makao hayo ya kimbinguni siku moja yatakuwa yangu.

Kwa hiyo, hema ama kibanda, kwa nini nijali?

Wao wananjengea jumba la kifalme kule!

La vito vyekundu na almasi, na fedha na dhahabu,

Makasha yake yamejaa, Yeye ana utajiri usiojulikana.

Loo, neema ya ajabu! jinsi inavyosikika tamu, Iliyomwoko mwovu kama mimi!

Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana,

Nilikuwa kipofu, bali sasa naona. (Hakuna nilichofanya.)

Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu kuhofu,

Neema ndiyo iliyofariji hofu yangu;

Jinsi neema hiyo ilivyoonekana kuwa ya thamani

Kwenye ile saa niliyoamini!

⁶³ Kujua ya kwamba ilikuwa si kitu ningeweza kufanya, ama ningefanya, ama nilichokuwa na wazo, ama nilichokuwa na majaliwa ya kufanya. Ni kile Yeye alichonifanyia. Yeye alishuka akaja akanikomboa, akaniweka kwenye ile Barabara Kuu; ndipo akasimama kwenye ile ncha nyingine, apate kuvuta pande zote pamoja, kufanya Milele isiyo na minyororo iendele. Nina haki ya kutembea katika Umilele huo kwa sababu Yeye alikufa na, mahali pangu, akaondoa dhambi yangu. Jambo la ajabu sana!

...torati, kwa kuwa ni kivuli—kivuli cha mema yatakayokuwa...

⁶⁴ Kivuli ni nini? Kivuli ni kitu kilichofanywa na kingine na kutupwa mbele yake. Mnajua, mara nyingi watu hunukuu Zaburi 23. “Naam, nijapopita kati ya vivuli vyeusi vya bonde la mauti.” Hilo ni kosa. Ilisema wao... Hapo, “Naam, nijapopita kati ya uvuli,” si uvuli mweusi. Kama kulikuwa na giza, kusingetokea uvuli. Hakuna budi kuweko na asilimia fulani ya nuru, kutupa uvuli mbele.

⁶⁵ Kwa hiyo, torati ilitoa nuru ya kutosha kuona uvuli wa kitu halisi kitakachokuja. Kristo alikuwa amewakilishwa katika torati hiyo, ya uvuli.

⁶⁶ Yeye alikuwa amewakilishwa, akatangulia kuonekana, katika Yusufu, chini ya torati. Yusufu, akiwa ni kivuli cha Kristo, alipendwa na baba yake, kwa maana alikuwa mtu wa kiroho. Yeye aliona maono, akatafsiri ndoto. Wa kiroho sana, naye akachukiwa na ndugu yake. Anafanana, na Kristo. Yeye aliona maono ya baba, naye alikuwa mtu wa kiroho. Naye ndugu yake alimchukia, bila sababu. Naye alidhaniwa kuwa ameuawa, nguo yenye damu ilirudishwa na kuwekwa mbele za baba yake.

⁶⁷ Loo, jinsi lilivyo zuri! Loo, nikianza kwenye jambo hilo, sitaifikia somo hili. Ile nguo, iliyorudishwa kwa baba yake, yenye damu, ikiwakilisha mwanaye aliyekufa; Isaka. Na leo, joho la Bwana Yesu, maisha Yake yaliyotakaswa na Damu Yake iliyomwagika kwa ajili ya wenye dhambi, inasimama mbele za Mungu kama kumbukumbu ya kwamba gharama imelipwa. Mnaona jambo hilo?

⁶⁸ Naye aliuzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha, kama Kristo alivyozwa. Alitolewa kutoka katika handaki, shimo, alikotupwa. Naye Kristo, pia, alitolewa kaburini. Naye akawekwa mkono wa kuume wa Farao. Hakuna mtu angaliweza kwenda kwa Farao, ila kwa njia ya Yusufu. Tangazo lilitolewa, ya kwamba, Yusufu akitokea, ya kwamba watatangulia, watu wataenda mbele yake, wa kupiga makelele, wakisema, “Kila mtu na apige magoti, Yusufu yuaja.”

⁶⁹ Sasa, Biblia ilisema kwamba, “Kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri, Jina la Bwana Yesu.”

⁷⁰ Yeye aliweza kuwafunga watumishi wa Farao apendavyo. Yeye alikuwa amepewa nguvu zote na mamlaka yote ya Misri

mikononi mwake. Na wakati magari yalipokimbia barabarani; kila mtu, wakati sauti ilipopazwa, kila Mmisri, haidhuru walimchukia vibaya namna gani, walimpigia Yusufu goti.

⁷¹ Siku moja, ewe rafiki mwenye dhambi, haidhuru unataka kuliita jambo Hilo “ushupavu wa dini” namna gani, haidhuru unataka kusema ni makosa namna gani, ni kiasi gani unataka kujinyonganyonga mwili na kuishi ulimwenguni, na kulidharau Kanisa na mambo ya Mungu, siku moja utapiga goti lako upende usipende.

⁷² Lakini linaweza kuwa jambo lenye utukufu namna gani kwa wale wanaompenda Yusufu. Jinsi walivyompenda, kasema, “Loo, huyu hapa yule mtawala mkuu anakuja, Yusufu.” Nao wakapiga magoti yao, na kusema, “Loo, Yusufu, uliyaokoa maisha yetu. Tungalion njaa hata tufe, kama isi- . . .”

⁷³ Lakini, hao wengine, hawakulithamini, “Ah, upuuzi!” Hawana shukrani. Tuna watu wa aina hiyo ulimwenguni leo. Hamtambui ya kwamba mkate mnaokula, na hewa yenyewe unayovuta, inatokana na Mungu. Nao wakamwabudu.

⁷⁴ Hapa si muda mrefu uliopita, wakati Bw. Baxter alipokuwa meneja wangu. Wakati Mfalme wa Uingereza . . . tulipokuwa kule matembezini. Wakati malkia alipotoka nje, bibi mzuri wa kupendeza sana, huku amevalia vazi lake maridadi, nywele zake zilizokuwa zinaota mvi. Naye mfalme ameketi, mgonjwa sana wakati huo, ilikuwa vigumu kwake kuvumilia. Alikuwa anaumwa na tumbo na ukavu wa mwili. Hiyo ilikuwa tu kabla hajaombewa. Bali ilikuwa ni vigumu kwake kusimama. Lakini, hata hivyo, ile damu yake ya kifalme, alifutua kifua chake mbele kidogo alivyoweza kuvimbisha, naye akapita barabarani kwenye gari la kusukumia.

⁷⁵ Bw. Baxter akisimama pale. Na wakati alipopita, nikamwangalia. Mdomo wake ulikuwa unachezacheza, manjozi yalikuwa yanatiririka mashavuni mwake. Akanikumbatia kwa mkono wake, kasema, “Ndugu Branham!”

Nikasema, “Naam, Ndugu Baxter?”

Akasema, “Unajua, mimi ni—mimi ni Mkanada.”

“Naam.”

⁷⁶ Akasema, “Mtu anayeitawala nchi yetu, mfalme, yeye na bibi-arusi wake mzuri mke wake, anapita. Hapo ndipo siwezi kujizuia. Sina budi kujiachilia.”

⁷⁷ Nikamkumbatia kwa mkono wangu, nikasema, “Ndugu Baxter, kama Mkristo, pamoja nawe, itakuwa vipi siku moja yenye utukufu, wakati Mfalme atakapokuja na Bibi-Arusi Wake!”

⁷⁸ Kama mtu angeweza kuwazia jambo hilo anapomwona mfalme wa duniani, ambaye ni mtu anayepatikana na mauti kama tulivyo sisi, itakuwaje tutakapomwona Mfalme wa

wafalme akija katika Utukufu? Jinsi utakavyokuwa wakati wenye utukufu!

⁷⁹ Yeye alionyesha katika kivuli hapo awali katika Yusufu. Alionyesha katika kivuli hapo awali katika Daudi. Torati ilimwonyesha hapo awali Kristo katika kivuli. Daudi . . . Kristo akiwa mwana wa Daudi. Halafu wakati . . . Kristo akiwa katika Daudi, kama kivuli, ilimfanya Daudi, alipokuwa ametolewa mamlakani, amekataliwa na ndugu zake mwenyewe; si ndugu zake mwenyewe tu, bali ukoo wake mwenyewe, Absalomu, na watoto wake mwenyewe. Hii hapa. Wao walimdharau baba yao wenyewe, na kuitaka damu yake, na kumtoa mamlakani. Ndipo akapanda kilima, Mlima wa Mizeituni, akiangalia nyuma, akiulilia Yerusalemu.

⁸⁰ Jinsi ambavyo Yeye, Mungu, alivyomwonyesha awali Kristo kwa kivuli katika Daudi. Kwa kuwa wakati alipotolewa mamlakani, akafukuzwa, na wajumbe wake mwenyewe, watu wake mwenyewe, Wayahudi, waliililia Damu Yake. “Hatumtaki Mtu huyo!” Yeye aliketi juu ya mlima wa Mizeituni na kuangalia Yerusalemu na kulia, akisema, “Yerusalemu, Ee Yerusalemu, jinsi ningewakusanya pamoja kama kuku avikusanyavyo vifaranga vyake, lakini hamkutaka.”

⁸¹ Kristo alionyesha kwa kivuli awali na Melkizedeki, katika ukuhani, katika sura ya a . . . katika sura ya 7 ya Waebrania. Jinsi ambavyo Melkizedeki . . . Ibrahimu pia alimwonyesha awali kwa kivuli, kule kote nyuma, mambo yote mazuri, kivuli tu. Na jinsi ambavyo Melkizedeki, katika sura ya 7, tunasoma habari Zake hapa. Tutasoma jambo Hilo tu kwa muda kidogo.

Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki;

⁸² Amina! Ibrahimu! Lutu, binamu yake, alikuwa amerudi nyuma. Mnaona Roho halisi na wa kweli wa Kristo? Natumaini mnalipata. Haidhuru alikuwa amerudi nyuma jinsi gani; alipokuwa katika shida, huyu hapa Ibrahimu anamjia, pamoja na jeshi. Wale wageni waliomzunguka, katika mabonde ya Sodoma, walikuwa wameshuka na kuuteka Sodoma na mfalme wake. Na kuchukua, humo, wakamchukua Lutu mateka.

⁸³ Naye Ibrahimu, mjomba wake, wa ukoo wake, watoto wa nduguze. Basi aliangalia huku chini akaona ya kwamba adui alikuwa amemteka mtu wa ukoo wake. Akaunda jeshi la watumishi wake mwenyewe, akaenda kumtafuta.

⁸⁴ Huyo alimwakilisha Kristo. Wakati alipoona Kanisa la Mungu aliye hai lilikuwa limetekwa, katika kosa la Ibilisi, Yeye aliunda jeshi la Malaika akaja duniani, kumfuatilia Ibilisi, akamshika. Haleluya! Tawanya adui! Loo, jinsi tunavyompenda kwa ajili ya jambo hilo! Akamshika adui. Naye akamwua

huyo adui, na kumnyang'anya kila kitu alichokuwa nacho; akamwondolea mbali.

⁸⁵ Na jambo la kwanza walilofanya lilikuwa nini, Ibrahimu akirudi pamoja na Lutu, mkewe, watoto wake, na mali yote, kwa ushindi wakirudi kwenye maskani yao ya zamani tena? Yeye alimlaki Melkizedeki.

⁸⁶ Melkizedeki alikuwa mfalme wa Salemu. Salemu ni Yerusalemu. Wakati Wayahudi walipoingia Yerusalemu, wao waliuita “J-...-u-salemu,” Yerusalemu. *Salemu* ambalo maana yake ni, “mji wa amani.” Yeye alikuwa mfalme wa... Sikilizeni. Hebu tulisome.

Ambaye... Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote;... likitafsiriwa ni falme wa haki,...

⁸⁷ Mfalme huyu aliyemlaki alikuwa nani? Akirudi kwa ushindi, na ushindi, kama Kanisa lilivyo leo, kutoka Kalvari.

...tena, Mfalme wa Salemu, maana yake, Mfalme wa amani;

Hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake,...

⁸⁸ Huyu Mfalme wa Salemu alikuwa ni nani? “Yule Mfalme mkuu wa Yerusalemu,” si ile ya duniani, ya Mbinguni. Yerusalemu ya duniani ni mfano wa ya Mbinguni.” Na hapa anakuja Mfalme wa Salemu, ambaye kwanza ni Mfalme wa haki, Mfalme wa amani; Yeye hakuwa na baba ye yote, hakuwa na mama ye yote; hakuwa na mwanzo wa uhai Wake, wala mwisho wa siku Zake.” Loo, jamani! “Bila wazazi.” Si mwingine ila Kristo Mwenyewe! Huyu ndiye Kanisa litakayemlaki litakapopaa hewani.

⁸⁹ Basi wakati Ibrahimu alipokutana Naye, yeye alimpa fungu la kumi la vyote alivyokuwa navyo.

⁹⁰ Mnajua walichofanya? Jambo la kwanza walilofanya lilikuwa ni kuketi chini. Ninajisikia nina msisimko wa furaha kwelikweli. Wakaketi wakaumega mkate, wakanywa divai, na wakafanya ushirika, baada ya vita kwisha.

⁹¹ Nayo Biblia inatwambia, Yesu Kristo alifanya, ya kwamba tuta-... “Sitakula kabisa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokula mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba Yangu.”

⁹² Ya kwamba, baada ya kupiga vita vya mwisho, na ushindi umepatikana, na waliopotea wamerudishwa kwenye Ufalme wa Mungu, tutaketi chini katika Ufalme wa Mungu, na pamoja na Melkizedeki wetu, Ambaye hana mwanzo wa siku Zake, wala mwisho wa miaka yake. Loo, jamani! Yeye ni Yeye asiye na minyororo, Aliye wa Milele, tutakula ushirika tena pamoja Naye.

⁹³ Loo, ni picha nzuri namna gani Agano hili la Kale la ajabu sana linatoa kwa waumini wa Agano Jipya. “Kwa kuwa torati ni kivuli cha mema yatakayokuja, wala si . . .” Sikilizeni. “Kwa kuwa torati ni kivuli cha mambo mema yatakayokuja, wala si sura yenyewe ya mambo hayo.” Ilikuwa ni kivuli cha sura.

⁹⁴ Daudi aliutawala ulimwengu, katika wakati wa heri na ufanisi wa Israeli. Yeye alikuwa nini? Kivuli. Daudi akiketi kwenye kiti cha enzi, ulimwengu mzima miguuni mwake, hicho kilikuwa ni kivuli cha nini? Ilikuwa kivuli cha kitu Fulani, kilichomfunika Mwana wa Daudi, ambaye ni Mwana wa Mungu, Ambaye ni Melkizedeki, “ambaye mwanzo wa siku Zake na mwisho wa miaka Yake, Yeye hana.” Kivuli cha, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, Yeye ataketi kwenye kiti cha Enzi cha Daudi na kuyatawala mataifa yote.

“Kivuli cha mambo mema.”

⁹⁵ Ni kitu gani leo? Tunaangalia na kuona kivuli, wanaume na wanawake wanaokiri kuwa ni Wakristo, nao wanaishi kama ulimwengu. Wao wanasema, “Loo, mimi ni mfuasi wa kanisa. Inaleta tofauti gani?” Ni kivuli cha mdanganyifu, tokea bustani ya Edeni, aliyejifanya kwamba ni mzuri, aliyejifanya kwamba ana Nuru, aliyejifanya kwamba ana hekima, bali alikuwa ni mdanganyifu. Na hivyo ndivyo wanaume na wanawake wanafanya leo, wanaoliita Jina la Yesu Kristo wala hawaachi dhambi, wakionyesha awali mfano wa hukumu watakayopata pamoja naye ambaye ni mdanganyifu. Yesu aliwaambia wale Mafarisayo watawa wa kidini, “Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi.” Natumaini mtaliona. Natumaini litaingia ndani kabisa. Kivuli cha udanganyifu.

⁹⁶ Basi vipi huyo Mkristo halisi, mwaminifu, asilimia mia moja, ambaye amezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, ambaye jina lake limeandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu? Ambaye . . . Yaje, yaende, yo yote yale, wao wanashikilia kwenye mkono wa Mungu usiobadilika. Ni kitu gani moyoni mwao kinachoonea njaa kitu fulani kule ng’ambo? “Kwa maana hao,” Biblia ilisema, “wafanyao maneno kama hayo, wanakiri wazi kwa ushuhuda wao, na maisha yao, ya kwamba wao wanautazamia Mji ujao, ambaye mwenye Kuujenga na mwenye Kuubuni ni Mungu.”

⁹⁷ Hiyo njaa moyoni mwako ni ya nini, asubuhi ya leo, kutaka kusimama katika Uwepo Wake? Hiyo njaa moyoni mwako ni ya nini, asubuhi ya leo, ukijitahidi kwa yote yaliyo ndani yako? Nafsi yako yote na maisha yako yote yanalilia jambo fulani, mpaka unasema, “Sijali kijacho ama kinachokwenda.”

⁹⁸ Ee Mungu! Kitu fulani ndani yako, kikiutazama ulimwengu, na machozi yanatiririka moyoni Mwako. “Loo, ewe ndugu uliyepotea!” Kuona wanawake katika njia yao duni, na iliyopotoshwa. Na kuona wanaume wakinywa pombe, na kuvuta

sigara, na kulaani, na kucheza karata; huku wanaenda kanisani. Ni kitu gani moyoni mwako kinacholia kwa sauti kuu, “Ndugu yangu mpotovu, uliyepotea”?

⁹⁹ Umegusa Kitu fulani *Hapa* juu. Umeunganishwa na upande ule mwingine wa kamba. Umegusa m—mnyororo, Barabara Kuu, iliyunganisha Umilele hapo mwanzo. Wakati jina lako lilipoandikwa kule, na kuonwa na ile sifa kuu, ama juhudi za maarifa ya Mungu yaliangalia chini na kuona ya kwamba ungekuja Nyumbani. Na, hata hivyo, huku umepofushwa na mambo ya ulimwengu huku chini, una wazo fulani. Wakati Roho Mtakatifu anapotelemlsha mnyororo huu wa damu, na kuukamata moyo wako, unanena juu ya Nchi bora zaidi, na Mahali pazuri zaidi, na Mji mzuri zaidi. Kwa hiyo, unaweza kusema:

Ulimwengu huu si maskani yangu,
Mimi ninapita tu;
Hazina yangu yote imewekwa kule juu,
Mbali sana ng'ambo ya mbingu.

¹⁰⁰ Mungu akizungumza. Na yaje, yaende, yo yote yale; moyo wako ungali umeimarishwa. Ni kivuli, kivuli kiko mbele yako. Hicho ndicho kinachofanya kivuli. “Kwa kuwa torati ni kivuli” cha ubatizo wa Roho Mtakatifu. “Kwa kuwa torati ni kivuli.” Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, katika Biblia, huna budi kuchukua na kulinganisha Maandiko kwa Maandiko, na kuyafanya yaambatane. Na kama yakipatana, pengo moja ndani yake, kumbuka, umetoka nje. Dumu kwenye njia hiyo, m—mstari huo wa Maandiko.

¹⁰¹ Sasa, “Kwa kuwa torati ni kivuli, haiwezi kumkamilisha mwabudu, haiwezi kumkamilisha akaribiaye. Kama ndivyo . . .” Sikilizeni, aya ya 2. Tutaijaribu, dakika tano zifuatazo. Angalia.

Kama ndivyo, je! dhabihu haingekomama kutolewa; . . .?

¹⁰² Kama damu ya mafahali na mbuzi na kondoo na ndama, na iwapo huyo kuhani mkuu alikuwa wa zamu ifaayo, basi ulimwengu ungalizidi kuendelea. Mauti yangelikwisha chini ya hiyo. Mumelipata? Hebu lingie ndani kwa muda kidogo. Kama Kayafa, kuhani mkuu, kule kutolewa kwa uhai wa mnyama, kungemkamilisha huyo mtu na kumpa Uzima wa Milele, basi hapakuwepo na sababu ya kitu kingine kutukia. Hiyo ingaliendelea moja kwa moja. Uzima wa Milele ungalianza, na kuendelea moja kwa moja. Bali ilibidi kuweko na kivuli cha Mwana-Kondoo halisi wa Mungu ambaye anakuja kuichukua dhambi ya ulimwengu, ambaye alinenwa hapo awali na Mungu.

¹⁰³ Nao wanaume na wanawake leo, ambao Mungu alitangulia kuwajua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Kama wakipaza sauti, sawa. Kama hawapazi, sawa. Kama wakifanya jambo *hili*, sawa. Kama hawafanyi, sawa. Kwa kuwa,

Mungu tayari amesema jambo hilo. Halina budi kutimia. “Si yeye atakaye, wala yeye apigae mbio, ni Mungu arehemuye.” Chaguo la Mungu, si letu.

¹⁰⁴ Sasa angalia. “Je! basi dhabihu hizo hazingekoma kutolewa? Kwa maana hazingekoma kutolewa? Kwa maana...” Kwa nini? Hapa tunakaribia kufunga sasa; shule imeondoka. “Kwa maana mwabudu...” Kwa nini? “Kwa maana...” Loo, ninajisikia kama mtoto mdogo akiwa na kitu cha kuchezea cha Krismasi sasa. Mimi nina furaha sana juu ya jambo Hili. Jinsi ninavyopenda kulipa Kanisa jambo Hili, kwenu ninyi waamini, kuwafanya mwone yaliyo Kweli! Kama zingalikuwa sawa, basi haingalikoma kutolewa; ingaliendelea, Uzima wa Milele. “Kwa maana mwabudu...” Sasa someni Hilo pamoja nami, “Mwabudu akiisha...” Si kila ufufuo, mpaka kila Jumapili asubuhi.

...lakini mwabudu *akiisha kusafishwa mara moja, asingejiona...kuwa ana dhambi.*

¹⁰⁵ Ati nini? “Mwabudu akiisha kusafishwa mara moja.” Kusafishwa na Damu ya Mwana-Kondoo, akisha kusafishwa mara moja kabisa, akitakaswa kabisa mara moja, humsafisha mwabudu, ile dhamiri ya dhambi imekwisha. Wazia jambo hilo.

¹⁰⁶ Neno *dhamiri*, katika tafsiri ya kweli ambayo tungetumia hapa. Hii ni nakala ya King James. Katika Uingereza, inamaanisha dhamiri fulani. Hapa, ingemaanisha “tamaa.” “Mwabudu akiisha kusafishwa mara moja,” kwa kusafishwa kwa Kristo Kalvari, “hawana tamaa ya dhambi tena. Mambo ya zamani yamepita; mambo yote yamekuwa mapya.”

¹⁰⁷ Sasa, unaweza kuimba kama ndege mwenye sauti tamu sana, na hata hivyo uwe na chuki, ghadhabu na ugomvi mwilini mwako, nafsini mwako. Unaweza kupiga makelele kama sijui nini, ungali unayo. Unaweza kucheza katika Roho, ungeweza kunena kwa lugha, unaweza kutabiri, unaweza kuhubiri, yo yote ya mambo hayo, na ungali una ghahabu, husuda, ugomvi moyoni mwako.

¹⁰⁸ Lakini kuchaguliwa tangu zamani halisi na kwa kweli kwa Neno la Mungu la Milele, na jina lako liliandikwa mle, na Damu ikipata kumtakasa mtu huyo; wazo lenyewe la jambo hilo, humhukumu papo hapo anaposimama.

¹⁰⁹ Kasema, “Usinihukumu. Ninaenda sehemu hizi; jambo hilo halinihukumu.” Kwa nini halikuhukumu? Wewe, kama mwabudu wa kivuli hujasafishwa bado kwa Damu ya Yesu Kristo.

¹¹⁰ Nao waishio kwa sheria wanashikilia wazo hili, “Haleluya, mimi nitavaa nguo yangu mpaka *hapa* chini, na nguo zangu chini *hivi*. Nitaachilia nywele zangu ziwe ndefu, nami nitakuwa sawa.” Huo ni uongo. Nao wanamwelekezea kidole mwanamke aliye na nywele fupi, na mwenye nguo fupi, na kusema,

“Yeye anaelekea jehanum.” Mimi siwezi kusema hivyo. Lakini ninafikiri mambo hayo ni sawa. Mimi siwahukumu. Bali wakati unapoweka matumaini yako ya Milele na wokovu juu ya fundisho hilo, umelaaniwa pamoja nalo.

¹¹¹ Mwanamume ama mwanamke, haidhuru kama wewe ni *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*, njoo kwenye chemchemi iliyojaa Damu iliyotolewa kutoka kwenye vena za Imanueli, na uruhusu Damu itakasayo ya Bwana Yesu Kristo ikusafishe dhambi zako.

¹¹² Ndugu, haidhuru, ungali unaweza kurefusha nguo zako sana, ungeweza bado kutovalia shati lenye mikono mifupi, ninyi wanaume, na mambo hayo, ama lo lote unalotaka kufanya; bali kama ungali una uovu, na wivu na ugomvi. Huenda ikawa ulikimbia, ukacheza, ukanena kwa lugha, ukapiga makelele, ukahubiri Injili, ama cho chote, bali umepotea mpaka damu hiyo imekutakasa na kukuweka katika upendo wa Kiungu wa Bwana Yesu Kristo, katika moyo wako, na kuacha nyayo za Maisha ya Kristo nyuma yako. Amina.

¹¹³ “Zikiwepo lugha, zitakoma. Ukiwepo unabii, utabatilika. Yakiwepo maarifa, yatabatilika. Lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika.”

¹¹⁴ Nasi tunasimama leo, kama wafuata sheria, juu ya jambo fulani la kisheria tulilotenda. Mbona, nilipokuwa mwenye dhambi, nilikuwa chui. Jinsi nilivyojaribu kuacha jambo *hili* na kuacha jambo *lile*, niliyafanya tu madoadoda yangu yang’ae zaidi. Nilikuwa mnafiki kwa jambo hilo, nawe pia. Bali siku uliyokuja Kalvari, kusafishwa, ambako yule Mwana-Kondoo halisi . . .

¹¹⁵ Chini ya Agano la Kale, wao walileta mwana-kondoo. Wao wangetoka waende wakafanye uzinzi. Wangeshikwa na hamaki, na kuzozana, na kupigana, na kutukana. Na, walipofanya jambo hilo, walileta mwana-kondoo, wakamleta kwa kuhani, wakasema, “Loo, ewe kuhani wa Mungu!”

“Naam?”

¹¹⁶ “Nilimlaani jirani yangu. Ni—nilifanya uzinzi. Nilisema uongo. Niliiba.” Anaweka mikono yake juu ya mwana-kondoo huyu anayekufa, bila waa. Kuhani akamchunguza; ilibidi awekwe, kuona kama alikuwa sawa. Akaweka mikono yake juu yake, ndipo wakakata koo lake. Nayo damu ikamwagika kwenye mikono yake, huku maskini mwana-kondoo yule analia, anarusha miguu, anakufa.

¹¹⁷ Naye mwabudu akisimama pale, alisema, “Naam, huyo inapaswa kuwa ni mimi, bali mwana-kondoo anapachukua mahali pang’u.” Lakini alirudi akiwa na tamaa ile ile. Yeye angerudia jambo hilo mara tu alipopata nafasi.

¹¹⁸ Na hivyo ndivyo watu wanavyofanya leo. Wao wanakuja na kukiri, na kusema, “Nina *hili*, *lile*, ama lile *lingine*,” nao wanarudi; kisha wanageuka, wanafanya jambo lile lile tena.

Wanajiunga na kanisa, lingine; kama hili likianzisha jambo fulani dogo, vema, wanaenda kwa *hili* na *lile*.

¹¹⁹ Bali hilo lilikuwa kivuli cha nini? Haikuwa imekamilika. Hiyo haingaliondoa dhambi kamwe, bali ilikuwa ni kivuli cha ile tiba halisi maradufu ijayo.

¹²⁰ Na wakati Yesu Kristo Mwana wa Mungu alipokuja, na akafa Kalvari, naye mwabudu mara moja anaweka mikono yake juu ya kichwa cha Bwana Yesu, na akijua ya kwamba kule kupiga makelele na kulia msalabani, yale mauti, yale mateso kwa ajili yetu, anapaswa kuilipa yeye mwenyewe, katika kilindi kile cha jehanum ambako alipaswa kwenda. Yeye alijua ya kwamba Kristo alilipa mahali pa kukiri dhambi yake.

¹²¹ Ndipo nini kilichotukia? Ni nini kilicholeta tofauti? Ni nini kilichotoka kwenye huyo mwana-kondoo, kutoka kwenye ile damu? Uhai ulitoka. Nayo chembechembe ya damu ilikuwa mikononi mwake. Uhai ulikuwa ukizungukazunguka madhabahuni, bali uhai wa mwana-kondoo usingeweza kumrudia mwamini; ingawa alikiri ya kwamba alikuwa amekosea, na mwana-kondoo alipachukua mahali pake. Kwa maana, mwabudu ana nafsi, wala asingeishi kama mnyama. Sawa.

¹²² Lakini, Ee Mungu, fyatua nyundo zote mbili kwenye bunduki, na ujalie mitutu yote miwili iende kwenye kanisa hili, ndilo ombi langu. Lakini wakati mwabudu. . .

¹²³ “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, Roho Mtakatifu. Hataingia hukumuni, bali amepita mautini kuingia Uzimani.”

¹²⁴ Wakati mwabudu anapoweka mikono yake juu ya kichwa cha Mwana-Kondoo wa Kalvari, na kukiri dhambi zake, na Mungu anatambua jambo hilo kuwa ni kweli kutoka moyoni mwake. Yeye hukiri dhambi zake. Huo Uzima unaozungukazunguka, unaoitwa Roho Mtakatifu wa Yesu Kristo, unageuka unamrudia mwabudu. Naye amesafishwa, wala hana tamaa ya dhambi tena. Kwa kuwa yeye anaongozwa na Roho wa Mungu, wala si uzima wake mwenyewe, tangu wakati huo na kuendelea. Yeye atafanya makosa, bila shaka, bali Uzima huo utamshikilia.

¹²⁵ Angalia. Hebu twende kwenye ninii ya nne. . . aya ya 14. Hatuna wakati wa kuimaliza. Hebu tuchukue aya ya 12.

Lakini huyu mtu, (si mwana-kondoo) . . . Kristo!

Lakini huyu mtu. . .

¹²⁶ Yeye anazungumzia sasa juu ya huduma ya ukuhani mkuu. Jinsi kuhani alivyoenda hekaluni, na kadhalika; kuabudu. Jinsi mwabudu alivyorudi akiwa na tamaa ile ile. Mtu anakuja madhabahuni na kusema, “Naam, sitaki kwenda jehanum.” Mhubiri akihubiri jinsi jehanum ilivyo na joto, na madhabahu

yamejaa watu. “Eee Mungu, sitaki kwenda jehanum.” Lakini wao hawataki kamwe kuutiisha huo ubinafsi, kusema, “Naam, Bwana. Si mapenzi yangu, tangu sasa na kuendelea, bali mapenzi Yako.”

¹²⁷ Kweli utambue yale unayofanya. Useme, “Mungu, unirehemu.” Damu ya Yesu imo mikononi mwako basi. Usitoke uende ukaishi maisha yale yale uliyoishi. Damu hiyo itakuhukumu mwishoni, kwenye ile Hukumu. Afadhali uwe na Uhai ulio katika Damu hiyo, uurudie uhai wa damu yako, urudi moyoni mwako na kukufanya uishi maisha tofauti ya Mkri- . . . mtu tofauti. “Mwabudu akiisha kusafishwa mara moja.” Angalia hapa.

Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo (muda gani?) hata milele, (Milele hiyo isiyo na mnyororo) . . . aliketi mkono wa kuume wa Mungu. (Kwenye kikomo.)

¹²⁸ Yeye yuko wapi? Kwenye kikomo. Mnakumbuka, Jumapili ya juzi, ile Jumapili niliyohubiri na kueleza kwa mifano kile kijisafina cha Musa, kilichokuwa kikienda kupitia kwenye manyasi na kila kitu? Mnakumbuka jinsi ninyi wazee mlivyolia na kupaza sauti, nilipokuwa nikiwahubiria watoto? Wote walikuwa na macho meusi na ya buluu, wakiketi hapa hapa kwenye safu ya mbele, nikiwaambia, “Ukiipoteza nafsi yako, utaipata. Ukiiponya nafsi yako, utaipoteza.” Mnakumbuka jambo hilo, enyi kanisa?

¹²⁹ Mnakumbuka, nilipokuwa nikieleza kwa mfano, nikatoa mfano wa asubuhi hiyo wakati Yokebedi na wakati Amramu, Haruni na Miriamu, wote wako kule chini kabla ya mapambazuko, huku wameinua mikono yao hewani, wakisema, “Mungu, Wewe ulitupa huyu mtoto, sasa tunakurudishia Wewe. Ulitupa sisi, hakuwa wetu, alikuwa Wako. Ulitupa sisi, na sasa tunakurudishia Wewe.” [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] “Tukimweka, wachawi wa jehanum watamwua.” Hao wanawake wenye pua ndefu zilizochongoka waje kule na kukikata maskini kichwa chake kidogo na kukivunjilia ukutani. Tutampoteza kama tukimweka. Bali kama tukimrudishia Yeye aliyetupa sisi, tutamwoko.”

¹³⁰ Hilo ni jambo lile lile ndani ya jahazi lako ndogo, asubuhi ya leo, ndugu, dada. Una shehena mle ndani, shehena ya thamani iliyopata kuweko. Inaitwa nafsi yako. Endelea, itunze, ishi utakavyo, utaipoteza hakika kama ninavyosimama hapa. Bali ukiirudishia Mungu, na kusalimisha mapenzi yako, utaiokoa. Utaipata. Yesu alisema hivyo. Kumbuka.

¹³¹ Na wakati walipoisukuma hii, hazina ya moyo wao, walipoisukuma wakaiingiza mtoni, huku maskini mamba wakija. Ninaweza kumwona Mungu, kama nilivyosema, akiinuka toka kwenye Kiti Chake cha Enzi.

¹³² Mwajua, kuna majaribu mengi yanayoendelea chini hapa. Bali kuna mtu Fulani anayeyaangalia, wakati wote. “Hawakuyapenda maisha yao hata kufa.”

¹³³ Wakati maskini mzee Amramu, akiwa na mtoto wake mdogo wa pekee, aliyempeda. Maskini Yokebedi alikuwa ndiyo kwanza amnyonyeshe kifiani mwake, halafu ilimlazimu kumweka katika safina na kuisukuma kuiingiza kwenye manyasi, ambako mamba walikuwa wamenenepa kwa kuwala watoto wachanga. Hapo, wakati alipokuwa amesimama pale, huku majoji yakitiririka mashavuni mwake, Mungu akasema, “Njoo hapa. Gabrieli, njoo hapa kidogo. Ninataka kukuonyesha jambo fulani. Nina mtu ambaye ananiamini Mimi kweli.” Amina.

¹³⁴ Mungu, nijalie niwe mtu wa namna hiyo, anayeweza kusema, “Mungu alisema jambo hilo. Ni kweli.” Nami niwe mfu sana kwa cho chote kile, hata kinakuwa shaba iliayo ama upatu uvumao.

¹³⁵ Kasema, “Njoo hapa, Gabrieli. Ninyi Malaika wote njoni hapa nje. Ninataka kuwaonyesha jambo fulani. Mnamwona mtu yule kule chini aliyeinua mikono yake juu? Alimsukuma akamtoa mwana wake mwenyewe nje. Nilimpa yeye huyo, sasa yeye ananirudishia. Nitahakikisha kwamba atamponya.” Amina. Kasema, “Gabrieli, waite Malaika elfu kumi, wape amri ya kuondoka. Ninawataka huku nje.”

¹³⁶ Gabrieli akapiga tarumbeta ndogo, nayo ikavuka ukumbi wa Milele. Malaika elfu kumi wenye silaha wakashuka.

¹³⁷ Kasema, “Jipangeni huku na huku mtoni. Mwone kwamba hakuna mamba, hakuna kitu kingine, kitakachomgusa mmoja wao. Yeye alirudishwa Kwangu.”

¹³⁸ Gabrieli akasema, “Bwana, Jemadari Mkuu, utakuwa wapi?”

¹³⁹ “Nitakuwa kwenye mwisho wa kamba. Nitapokea kule chini.”

¹⁴⁰ Hilo ndilo jambo lile lile analofanya leo. Wakati mtu anapoweka tumaini lake katika Bwana Yesu, anakiri dhambi zake, Roho Mtakatifu humshika mtu huyo, naye Kristo anasimama upande wa mwisho apate kumpokelea. Kupitia katika mizunguko ya maji, na mamba, na pepo wa kutisha, na cho chote kile tulichopitia.

Kwenye hatari nyingi, taabu, na mitego,
Tayari nimepitia;
Neema ndiyo iliyonileta salama umbali huu,
Neema ndiyo itakayonipeleka Nyumbani.

¹⁴¹ Ni nani aliye upande wa mwisho kupokea? Sikilizeni.

...hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu;

*Tangu hapo (huko ng'ambo mwishoni mwa njia)
akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya
miguu yake.*

¹⁴² Mko tayari? Hili hapa. Huu hapa mzunguko wa mwisho wa skrubu. Hii hapa sehemu ya mwisho ya tochi. Huku hapa kupigiliwa kwa mwisho kwa msumari. Huku hapa kupigiliwa kwa Milele kwenye Umilele. Na, mle ndani, Upanga wa ukombozi wa Mungu tayari umechoma moyoni, katika kuwasimamisha wajumbe Wake, kwa Roho Mtakatifu. Hili hapa, Waebrania 10:14. Sikilizeni. Si neno langu; bali ni Neno la Mungu, Ambaye alilinena kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Halina budi kuwa hivyo.

*Maana kwa toleo moja Yeye (a-m-e-w-a-k-a-m-
i-l-i-s-h-a) amekwishaamilisha hata milele hao
wanaotakaswa.*

¹⁴³ Kuwakamilisha kwa muda gani? Mpaka wakati mwingine utakapozozana na jirani yako? Mpaka wakati mwingine utakapomwona mtu fulani, mwanamume ama mwanamke ambaye ana tamaa mbaya? Mpaka wakati mwingine utakapopata nafasi ya kusema uongo mkubwa? Mpaka wakati mwingine utakapoweza kumtega mtu na kuwaudhi, na kuwafukuza kanisani, ili wakati mwingine uweze kumlaumu mtu fulani?

¹⁴⁴ "Yeye amewatakaswa milele, amewakamilisha milele." Ambapo Roho Mtakatifu...Huenda ukasema kitu fulani, wakati mwingine, kibaya. Hiyo ni kweli. Huenda ukatenda jambo fulani, wakati mwingine, baya. Hiyo ni kweli. Bali mara unapofanya hivyo...Angalia aya inayofuata.

Na Roho Mtakatifu naye...

¹⁴⁵ Loo, jamani, siwezi kuhubiri tena. Angalia.

...Roho Mtakatifu...anatushuhudia;...(Jamani!)

*...Roho Mtakatifu...anatushuhudia;..., maana,
baada ya kusema,*

*Hili ni agano nitakaloagana nao katika siku zile,
anena Bwana, Nitatia sheria yangu moyoni mwao, na
katika nia zao nitaziandika;*

*Ndipo anenapo, Dhambi zao na uasi wao
sitaukumbuka tena kabisa dhidi yao.*

¹⁴⁶ Ee Mungu! "Kila mwenye matumaini haya hujitakasa, kama Mungu alivyo mtakatifu."

Na tuombe.

¹⁴⁷ Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe, asubuhi ya leo, kwa ajili ya kusafishwa kwa Roho Mtakatifu, kwa ajili ya neema ya Mungu aliye hai. Sisi tulikuwa wenye dhambi, wasio na haki, wasio mcha Mungu, wasiopendeka; bila Mungu, bila

matumaini, tumetengwa na ulimwengu, ndipo Kristo akaja na kupachukua mahali petu. Kwa kutangulia kujua Mungu alituona katika hali hii, akijua ya kwamba tulikuwa na njaa na kiu. Si ajabu Yesu alisema, “Hao watashibishwa.” Si “kuwa wafuasi.” Si “hao watajiunga.” Lakini, “Hao watashibishwa; kuona njaa na kiu ya haki.” Kwa maneno mengine, “Kuona njaa na kuona kiu,” tukijua kwamba hatuwezi kufanya kitu sisi wenyewe, hata tufanye nini.

¹⁴⁸ Ibilisi anaweza kutufanya tuigize kila karama. Angeweza kutufanya tutoke twende tukaweke mikono juu ya wagonjwa, nao wangepata afya. Angeweza kutufanya tunene kwa lugha. Angeweza kutufanya tufasiri lugha. Angeweza kutufanya tuwe na hekima, maarifa. Lakini jambo hilo silo, Bwana.

¹⁴⁹ Wewe ulisema, “Wengi watakuja siku hiyo, na kusema, ‘Bwana, Bwana, sikufanya mambo haya kwa Jina Lako?’” Yeye akasema, “Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Hata sikuwajua ninyi kamwe.”

¹⁵⁰ Ee Mungu, basi hebu tumaini letu lijengwe si juu ya kitu ila juu ya Damu ya Yesu pamoja na haki.

Wakati yote yaliyo karibu na nafsi yangu
yanapoanguka,
Yeye ndiye tumaini letu lote na ngome yetu.
Kwa kuwa kwake Kristo Mwamba wenye
imara, nasimama,
Mahali pengine pote ni mchanga unaodidimia.

¹⁵¹ “Kumjua Yeye ni Uzima,” si kujua zile taratibu. “Kumjua Yeye,” Mtu.

¹⁵² Ninaomba, Baba, kwa ajili ya kila mwenye dhambi katika jengo hili leo, ya kwamba utawaokoa sasa hivi. Na naomba wao, bila mwamsho wo wote, bila mabishano yo yote kutoka kwa Ibilisi; lakini jalia wao, kwa imani ya kweli, isiyoghoshiwa, waamini yale waliyosikia yakihubiriwa, na kumkubali Roho Mtakatifu aliyelileta. Tujalie, Bwana, kwa maana ni katika Jina Lake tunaomba.

Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

¹⁵³ Sijui kama kuna mtu fulani hapa asubuhi hii. . . Sasa nataka ninii yenu. . . mwenzavyo, waaminifu, wakweli; haidhuru umejanya nini, haidhuru umeanza mara ngapi, ama umekuwa mfuasi wa kanisa muda gani. Hivi wewe ni mwaminifu, kutoka kwenye kilindi cha moyo wako, juu ya jambo hili, ambapo unajua ya kwamba mambo ya ulimwengu yamekuacha? Kujua ya kwamba, siku baada ya siku, na mwaka baada ya mwaka, inaendelea, nanga yako inashikilia? Kuna Mtu fulani, huko ng’ambo, ameonyeshwa mbele kwa kivuli kwenye mwisho wa njia, ambapo dosari hii kubwa itatolewa. Kuna Mtu fulani kule anayeuvutavuta moyo wako, ukijua ya kwamba siku moja

utainuliwa juu. Kama hilo halijatoka moyoni mwako leo, ewe rafiki, raia wenzangu, msafiri. . .

¹⁵⁴ Maskini kundi dogo, Mungu aubariki moyo wako. Kuwaona mmeketi hapa, wenye mvi na mabega yaliyoinama. Kuona maskini watoto wadogo, ambao labda iliwabidi kukosa chakula. Hivi ningesimama hapa na kusema jambo baya kwenu? Hilo, vema, Mungu apishe mbali! Ngingekuwa ninii. . . Inanipasa kupiga magoti na kutubu kabla hata sijahubiri. Ninawapenda. Na hilo ni kwa upendo halisi wa Kikristo.

¹⁵⁵ Iweni waaminifu sasa kwa Roho Mtakatifu. Hivi mambo hayo yote yamekuacha? Ama, Shetani amekudanganya, nawe unaishi tu maisha ya nusu-nusu? Wakati mwingine wewe unafikiri, “Vema, sawa,” na wakati mwingine, mbona, wewe, “Vema, sijui”? Na mambo yanatukia, ambayo unajua. Na kama hiyo ndiyo hali yako, basi, asubuhi ya leo, unataka kutoa yote kwa Kristo.

¹⁵⁶ Kumbuka yale aliyosema. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna, sasa hivi, Uzima wa milele.” Hukumu imekwisha. Tangu wakati huo na kuendelea, kitu hicho kitakuwa kimekufa. Kama kweli ukikubali jambo hilo, litajithibitisha.

¹⁵⁷ Sasa angalieni. Msidanganywe. Mnakumbuka hapa, miaka mingi iliyopita wakati tulipoliweka kanisa katika utaratibu? Ninazungumza nanyi, na mnaomba; vichwa vimeinamishwa. Kumbukeni wakati tulipoliweka kanisa katika utaratibu? Wakati ujumbe ulipotolewa katika unabii, ama katika lugha na kufasiriwa, wakati tulipouandika na kuuweka hapa jukwaani, umeshuhudiwa na watu watatu. Nilitoa ujumbe kutoka jukwaani. Kama haukutimia, mlikuwa na pepo mchafu kati yenu. Mlikuwa hapa mkatubu jambo hilo.

¹⁵⁸ Kama mtu fulani alifanya makosa, dada fulani ama ndugu fulani akiwaona wakifanya makosa, waliwaendea. Walipokuja kanisani, niliwashika mkono, tukarudi hapa chumbani, kasema, “Ndugu, nilikuona mahali pabaya. Sitasema jambo hilo kanisani, maana ninakupenda. Ulikosea. Hebu tuombe sasa.” Mnaona?

¹⁵⁹ Sasa uwe mwaminifu kwako mwenyewe. Kama upendo wa Kristo umo moyoni mwako, juu ya cho chote kile, Mungu akubariki; wewe uko sawa. Bali kama haupo, usidanganyike. Pepo hao ni wadanganyifu wawezavyo kuwa. Wanakudanganya. Hivyo ndivyo mmoja alifanya kwa Hawa, akamwambia ukweli mwingi sana mpya. “Loo, naam, Mungu amesema. A-ha. Bali kuna kasoro kidogo ndani yake. Hiyo ndiyo. . . Hiyo ndiyo iliyotuvunja asubuhi ya leo; tunaona kasoro ndogo kwenye mnyororo. Hiyo ndiyo inayosababisha shida zote.

¹⁶⁰ Ndugu, kama jambo hilo haliambatani kikamilifu na moyo wa Mungu, waweza kumwinulia Mungu mkono wako sasa,

na kusema, “Mungu, kwa huu, kweli nataka kuwa sawa”? Hakuna mtu atakayeangalia ila mimi. Inua mkono wako. Mungu akubariki, bibi. Mtu mwingine? Mungu akubariki. Mungu akubariki, nawe, nawe, nawe, wewe. Mungu akubariki. Sasa, Yeye anakujua. Yeye anamjua kila mmoja wenu. Anajua tu haja yako.

¹⁶¹ Sasa, njia yetu ya mtindo wa kale (huku mmeinamisha vichwa vyenu) ni kwa watu kuja madhabahuni. Hiyo ni sawa. Ninapenda jambo hilo. Hilo si jambo la Biblia. Hilo ni fundisho tu la kanisa.

¹⁶² “Wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika wana na binti za Mungu.” Wakati tu ukiwa umeketi, nawe umeinua mkono wako, dazan moja ama zaidi yenu hapa, mwaweza sasa kukubali, katika kilindi cha moyo wako, baada ya kusema unajisikia kwamba unapaswa? Mwaweza, kundi lilo hilo lililoinua mkono wako, waweza kuinua mkono wako, useme, “Nitakubali sasa jambo hili, Ndugu Branham. Sasa nitamkubali Yesu. Haidhuru nimefanya jambo gani, sasa namkubali Yeye kama Mpenzi wangu na Mwokozi wangu”? Mungu akubariki wewe, bwana. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mungu akubariki, bibi. “Sasa nitamkubali Yeye. Kitu fulani moyoni mwangu kikiinambia ya kwamba na—na—nataka kukubali. Kuna Kitu fulani kinachoniambia ya kwamba yanibidi, sasa hivi. Hii ndiyo siku yangu. Labda wakati mwingine, nitakuwa mbali sana.” Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, bibi. Ninauona mkono wako. “Sasa najisikia sharti nifanye jambo hilo.”

¹⁶³ Enyi marafiki, kanisa linakuwa baridi. Marekani itahukumiwa karibuni sana. Kila taifa lililipokea. Utakuwaje miaka mia moja tangu wakati huu? Utakuwa mahali fulani. Pengine kati ya dakika hii na miaka mia moja tangu sasa, utaondoka humu ulimwenguni. Afadhali uwe na hakika. Usichezecheze nalo. Neno linahubiriwa na Roho Mtakatifu, na ni Kweli inayotoka kwenye Neno la Mungu. Kuna Mtu fulani anayekupenda.

¹⁶⁴ Sasa, huwezi kuinua mkono wako, isipokuwa Mtu fulani alikuwa kuinua mkono wako. Huyu ni Roho Mtakatifu. “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Na kama Yeye anakupenda kutosha kubisha moyoni mwako, na kusema, “Naam, ninamaanisha wewe. Huu ndio wakati. Ninataka kuingia, kabla haijanilazimu kukuondoa kutoka dunia hii kabla ya wakati wako. Sasa nitakuomba uinue mkono wako.” Hivi hutafanya jambo hilo basi?

¹⁶⁵ Mtu mmoja zaidi aseme, “Mimi sasa, kutoka katika kilindi cha nafsi yangu, nalikubali”? Sasa nitawaombea. Mungu akubariki, bibi. Nilijisikia tu, dada mpendwa, ya kwamba huyo alikuwa ni wewe. Niliangalia kule nyuma... Bila shaka,

unatambua nimebakiza siku chache tu, masaa machache, kabla ya ule mkutano kule. Ninakaa chumbani mwangu sana sasa, nikiomba. Ibada ya kuponya: Malaika wa Bwana yu karibu. Mambo makuu yatatukia. Niliangalia nyuma nikaona Kitu fulani kimesimama chumbani, kilikuwa juu ya kijana mwanamke. Niliwaona wengine wakiinua mkono wao. Nilihisi ushuhuda ya kwamba jambo hilo ni kweli. Nikawaza, “Kama nikiita mara mara moja nyingine zaidi, kama mwanamke huyo atainua tu mkono wake.” Naye akainua. Jambo lilikuwa hilo.

¹⁶⁶ Sasa, Mungu, upendaye nafasi yetu, sisi ni nani, hata hivyo? Mbona, kabla ulimwengu haujapata kuumbwa, Wewe ulimjua kila mbu atakayekuwepo duniani, kila siwafu, kila tekenya. Wewe huna kikomo. Nawe ulijua ya kwamba, asubuhi ya leo, ya kwamba watu wangeinua mkono wao. Ulijua jambo hilo. Kwa nini, Wewe uliwaona kabla ulimwengu haujaanza. Umejua jambo hilo, daima. Nawe ulijua ya kwamba jambo hili lingetukia, kusudi upate kuonyesha upendo Wako kwa watu Wako. Ulisema ulimwinua Farao na kuufanya mgumu moyo wake, upate kuonyesha nguvu Zako, ni zaidi sana vipi utaonyesha upendo Wako! Shetani, huyo mwovu aliyepotosha kweli ikawa uongo, Wewe ulimruhusu kufanya jambo hilo, kwa sababu waweza basi kuonyesha upendo Wako kwa watu Wako. Na, Ee Mungu, tunakupenda sana! Tunakuthamini Wewe!

¹⁶⁷ Nami naomba, Mungu, ya kwamba watu hawa wataishi maisha manyenyekevu ya Kikristo, tangu leo na kuendelea, kwa kuwa wao wamekukubali Wewe. Na iwapo kuna wengine, labda sikuwaona wote, labda Wewe hukunionyesha mimi wao, bali umenena nao. Kama kuna wengine, wabariki pia. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Kuna chemchemi iliyojazwa damu,
Iliyotolewa kwenye vena za Immanueli,
Wenye dhambi wanapojitumbukiza chini ya
mafuriko hayo,
Hupoteza hatia zao zote...(Polepole sasa,
dada.)

¹⁶⁸ Mwajua, jana, Ndugu Roberson alikuwa kwa Ndugu Woods. Nilienda kule kisirisiri. Nilikuwa nikimngojea mhudumu aliyekuwa atanitembelea. Alitupa picha, nayo hiyo picha ilikuwa...Wengi walikuwa wakitazama, lakini, moja ya hizo, wakati kanisa lilipokuwa linatoka mlangoni. Nami nikajiona nikitokea pale, ndipo nikaangalia, “Loo, mie! Jamani, jinsi, gani miaka michache imekufanya wewe!” Ndipo nikaangalia tena. Jambo hilo likaja moyoni mwangu, asubuhi ya leo.

¹⁶⁹ Ni siku chache tu zaidi tuna taabu na dhambi. Nami nafikiria juu ya nyakati nilizosikia wimbo huo ukianza, nikawaona wakija hapa, kusimama madhabahuni kushiriki Meza ya Bwana. Nami nimesikia magurudumu ya sanduku

la kuzikia maiti yakilia kweche, lilipokuwa linashuka kuja chumbani pale, kuwaondosha.

¹⁷⁰ Kumbukeni, kuhubiriwa kwa Neno hili kutakuwa... Kutasimama Hukumuni. Nami itanibidi kusimama nyuma Yake, kusimama pale. Itanibidi kuwa shahidi wa jambo hilo. Siwezi kulighairi. Nimelinena. Sina budi kudumu nalo. Litakutana nami Hukumuni, kama tu Mungu alivyosema Neno Lake wala hawezi kulighairi. Mnaona?

¹⁷¹ Nami hupima kila neno, kwanza moyoni mwangu, na kuona kama nataka kulisema, mimi wenyewe. Kama linaelekea ni makosa, silisemi. Namwachia Yeye aliseme. Kama—kama Yeye akisema jambo, kinyume, ingawa nisingeliamini, nitalisema, kwa vyo vyote, maana ni Yeye. Nataka kuwa na hakika, maana sitaki makosa yo yote siku ile.

¹⁷² Mwajua, itakuwa giza sana, kule chini mtoni, siku hiyo. Hakutakuweko na mtu pale wa kusaidia. Hamtaenda na pesa kule. Marafiki wako watakuwa katika hali ile ile uliyomo; itakuwa giza sana. Hauna budi kuvuka. Ninataka kuhakikisha ya kwamba tikiti yangu iko sawa. Ninataka kuwa na hakika, nitakapoiangalia, ninaona Damu nyekundu ya Bwana wangu. Ndipo nitakaposikia, baada ya kitambo kidogo, ile meli ya zamani ikipiga honi, itakuwa sawa wakati huo. Lakini sitaki shida yo yote kule wakati huo. Nataka kulitatua jambo hilo sasa. Kama kuna shida yo yote, nataka itatuliwe sasa. Nitahitaji kila chembe cha neema ninachoweza kupata, kwenye siku hiyo.

¹⁷³ Nitakuwa mwaminifu. Kama vile mwalimu mkuu alivyosema, juzijuzi, hakutaka kupendwa na watu wengi, alitaka kuwa mwaminifu. Ninamuunga mkono. Ninataka kuwa mwaminifu. Ninataka kusema Kweli, ili kwamba kwenye siku hiyo, itakapokuja, nitakaposikia makelele ukingoni, ninataka kuangalia na kuwa na hakika.

¹⁷⁴ Kama watoto wa Kiebrania, walipoona hizo mbawa nyeusi zikipita, za mauti, mvulana mdogo alimuuliza baba yake, “Una hakika damu iko kwenye kizingiti?”

Baba yake akachungulia nje, “Naam, mwanangu, damu ipo.”

“Vema, hilo ni sawa basi. Sisi tu salama.”

Ati haiko, asubuhi ya leo, ewe rafiki? Hakikisha.

¹⁷⁵ Sasa, Ora May, najua umekuja kuombewa, dada. Maskini msichana huyu mdogo, jinsi alivyoketi hapa kwenye safu, kama mtoto mchanga. Pale, mtoto Shirley ameketi pale, analia, ndiyo kwanza atoke Arizona. Ninafikiri juu yao hao watoto wadogo. Nyote mnawakumbuka, huku nje katika nyumba ndogo—ndogo ya sanduku, maskini mzee baba yao anaketi pamoja nao kule nyuma humu kanisani, kwa ajili yao. Kumbukeni, hao jamaa wadogo jinsi mimi. . . jinsi sisi sote tunavyowajua. Jinsi maskini

Ora May...Inatakiwa watu wawili kulea jamaa. Ee Mungu, jambo hili la kuchukiza la ndoa na talaka. Na jinsi Curtis alivyojibidisha, kwao. Alifanya kazi kwa bidii. Lakini, mtoto, haidhuru yeye ni nani, anahitaji upendo wa mama. Mtu fulani wa kuwapenda. Ni maumbile, kutuliza moyo wako.

¹⁷⁶ Mimi ni mwindaji. Mimi huchunguza wanyama pori. Hiyo ni ninii tu...Nami hutoka nje na kuwachunguza tu. Mama mzee wa dubu, anapoingia, katika msimu wa kupukutika majani, yuko tayari kuzaa tena. Anawafukuza watoto wake wote. Yeye ana mmoja ama wawili; anawafukuza, anawafanya walale usingizi wa kupisha majira ya baridi, ili kwamba wazoe jambo hilo.

¹⁷⁷ Mwaka ujao, anapotoka nje, ana watoto wadogo wawili zaidi, mmoja ama wawili. Yeye huwalea katika msimu wa kiangazi. Halafu, kwenye msimu wa kupukutika majani, anawafukuza tena.

¹⁷⁸ Ana wawili tena msimu wa kiangazi unaofuata. Lakini vipi kama hatapata watoto wo wote mwaka huo? Mnajua analofanya? Anatoka nje, anajaribu kuwatafuta wale watoto, wao ni wakubwa kama alivyo yeye. Kama hawezi kuwapata, atawachukua baadhi ya mbwa mwitu wadogo. Atawachukua mbweha wadogo. Angemchukua, kweli, mtoto wa binadamu. Hakika, imetendeka. Atamchukua huyo mtoto mchanga, ama cho chote kile, na atamlea. Ni maumbile tu. Hawezi kujizuia.

¹⁷⁹ Mwangalie msichana mdogo akiwa na mwanaserere wake, mbona, yeye hafafikia umri wa miaka mitatu bado. Nilimwona mtoto wangu mdogo Sara, usiku wa juzi. Nilienda chumbani. Kijitu kidogo chenye wasiwasi, naye huyo pale, amelala na mwanaserere wake mkononi mwake. Nilisimama hapo nikaangalia chini. Nikawaza, "Maskini mtoto! Mnajua, haitachukua muda mrefu, miaka mingi, baba atazeeka, baada ya kitambo kidogo. Nimezeeka sasa; nipate mvi na kuaga dunia." Lakini huko ni kuonyesha mbele, siku moja, mtoto ha—halisi mchanga sana amelala pale." Limo tu ndani yako. Na iwapo huwapendi hao watoto wadogo, kitu kingine kitachukua mahali pake.

¹⁸⁰ Kama mtu hamwabudu Mungu, ataabudu gari lake, ataenda kwenye baa, a—atafanya jambo lingine, atazurura. Maana, kuna kitu ambacho hakina budi kupachukua mahali hapo.

¹⁸¹ Sasa, dada yetu, sitaki kumfanya ashikwe na mwamsho. Lakini, kwa kuwa hakupata malezi ya mama, vizuri, kitu kingine kilichukua mahali pake. Na maskini mtoto huyu anaugua, asubuhi ya leo, ugonjwa wa neva; watoto wawili wachanga. Yeye amefanya makosa; nami pia, na ni nani mwingine hajafanya? Lakini ninajaribu kusema, kuna Mtu fulani ambaye tayari amesamehe jambo hilo. Yeye aliinua mkono wake muda kidogo uliopita; yote yamekwisha. Jambo hilo lilitokana na

moyo wa kweli, ndivyo ninavyotaka kuamini hivyo; angalia tu litakalotukia. Wakati atakapokuwa mzee mwenye mvi, lingali litasimama. Hiyo ni kweli. Lakini, yeye ana wasiwasi.

¹⁸² Hakuna dawa ulimwenguni inayoweza kutibu wasiwasi. Kama ukinywa dawa, kutuliza neva zako, itakufanya mgonjwa mara mbili zaidi itakapoisha.

¹⁸³ Hakuna dawa ya wasiwasi, bali nina furaha sana kuna kuponya. Mnajua, nimeugua huo, pia. Kuna kuponya, si dawa; kuponya, kuponya maradufu.

¹⁸⁴ Katika somo langu jana, kwenye redio: *Kosa La Ukombozi*. Wahubiri wanahubiri juu-juu sana, kama Joash alivyofanya. Ilimpasa kugusia mengi zaidi.

Lakini, angalia, ndugu yangu, dada. Dawa ni Kristo.

¹⁸⁵ Ama, hebu niseme jambo hili, mimbarani, nyuma ya kijisanduku hiki cha kale kilichojengwa hapa; lakini ni kitakatifu tu kama mimbara yo yote ya Injili. Imewekwa wakfu kwa Mungu. Sisi ni maskini. Huenda isiwe na tabaka ya dhahabu juu yake, bali Roho Mtakatifu amekuja hapa na kutufanyia mambo makuu.

¹⁸⁶ Dada yangu, mpenzi, Mungu aubariki maskini moyo wako. Kama mama, na kama mtoto, kama utakubali yale Ndugu Bill amesema...ama anayokwambia sasa, nitakuhakikishia, mpenzi, ya kwamba utatoka hapa, utakuwa mzima.

¹⁸⁷ Sasa, ulipoinua mkono wako kitambo kidogo, wakati huo ulimkubali Kristo. Ninakutaka, katika dakika chache, nataka uje hapa. Nami ninaweza kukuthibitishia, kwa... Wewe, wewe uwe hakimu. Kwa neema ya Mungu, na Roho Mtakatifu anayesimama hapa, ninaweza kuufanya ukuache. Hiyo ni kweli. Sijaiona imeshindwa kamwe. Lakini basi utakurudia utakapoondoka hapa, unaona, kama utauruhusu. Lakini kama hutaubali tena, haidhuru unajisikiaje; endelea kusema, "Yesu Kristo huniponya."

¹⁸⁸ Unaona, umeshuka, Ora May, kutoka *hapa* juu, ambapo ulikuwa na furaha na kuendesha baiskeli ile, na kukimbia huku na huku barabarani hapa. Ulikuwa na furaha wakati huo. Hukuwa unajisikia unavyojisikia sasa, sivyo? Unaona? Sasa umeshuka *hapa* chini, ni kwa sababu hapakuwepo na kitu pale juu cha kukushikilia, mpenzi. Ulishuka *hapa* chini. Lakini sasa inakupasa kuamini ya kwamba uko *hapa* juu, na kuamini jambo hilo. "Na imani bila matendo imekufa." Kama unaamini jambo hilo, basi tenda kama kwamba uko hapa juu, ndipo Mungu atakuinua moja kwa moja pale juu tena.

¹⁸⁹ Huyu hapo shangazi wako Meda ameketi pale nyuma. Alikuwa na jambo lile lile. Nilikuwa na jambo lile lile. Ninajua ni nini, bali Mungu ndiye mponya.

Utaamini jambo hilo, asubuhi ya leo, Ora May?

¹⁹⁰ Ninataka uje hapa. Mtu mwingine ye yote yule kati yenu, aliye mgonjwa, kupakwa mafuta. Basi.

Na tuinamishe vichwa vyetu muda kidogo tu.

¹⁹¹ Kanisa, ninyi nyote mnamjua Curtis. Mnamjua Ora May. Ukimtazama tu Ora May, unaweza kuona jambo fulani limetukia. Yeye amechoka na amefadhaika. Ora May, huu ndio wakati wa kukata kauli.

¹⁹² Nilitaka kukuuliza jambo fulani. Mara nyingi, Ora May, umesema, "Laiti ningalipata mahali pa kuanzia. Kama ningaliweza tu kuanza wakati huu kujisikia vizuri zaidi, ninaamini ningejisaidia kujimudu." Unaona, hiyo ni kweli, sivyo? vema, uko mahali panapofaa sasa, Ora May. Uko mahali pazuri sana duniani, madhabahuni, ambapo Mtu pekee ulimwenguni anayeweza kukusaidia, atakusaidia, huyo ni Mungu.

¹⁹³ Ninawatakeni mwinamishe vichwa vyenu, kila mtu, muungane pamoja nami katika maombi.

¹⁹⁴ Baba mpendwa wa Mbinguni, wakati maskini msichana huyu mdogo... Maisha ni mafupi sana. Sasa yeye ni mama kijana. Ninajua, muda kidogo uliopita, alipoinua mkono wake, kila dhambi iliondolewa mbali. Mungu, Biblia Yako ni shahidi wa jambo hilo. Ulilinena kutoka Mbinguni, ya kwamba, "Yeye ambaye angeamini, angepokea."

¹⁹⁵ Sasa, yeye ana kazi ngumu sana mbele yake, Bwana. Naye Shetani angemtupa, huko mbali, na kumnyang'anya hao watoto, na kumlaza katika hospitali ya wenda wazimu, akakipigishe kichwa chake ukutani. Lakini yeye amekuja mahali panapofaa, leo, madhbahuni. Amekuja katika nyumba ya Mungu aliye hai. Amesimama hapa, kama ilivyokuwa, peke yake, madhabahuni, lakini si peke yake. Malaika wa Mungu wamefanya kituo kumzunguka. Roho Mtakatifu yu karibu, pia. Naye ni shahidi wa kuyaona mambo mengi yakitukia, na kujua ya kwamba Wewe ni Mungu. Nami naomba ya kwamba, kwa moyo wangu wote, kwa nafsi yangu yote, ya kwamba, siku hii, ya kwamba Wewe utamsaidia Ora May.

¹⁹⁶ Sasa, Baba, ninachukua kutoka kwenye madhabahu hii, ambayo yamewekwa hapa kwenye mahali hapa patakatifu ambapo Roho Mtakatifu amepatia uvuli... Yanaitwa mafuta ya mzeituni, ama mafuta ya kupaka, mafuta ya upako. Ni kulingana na agizo Lako, mafuta kutoka kwenye mzeituni wa tawi. Na sasa ninapoenda kumpaka dada yangu mafuta kwa mafuta haya. Wewe ulisema, "Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule." Baada ya kuhubiri Injili...

¹⁹⁷ Kwa kuwa tunajua ibada hii kubwa inakuja, mapenzi Yako yatendeke, hapa Indianapolis, ambapo watu wengi wenye ugonjwa mbaya wa neva, viziwi, bubu, vipofu, na kila kitu, watasimama pale. Lakini hatuogopi hata kidogo. Ulinena jambo

hilo, kabla ulimwengu haujaaza. Sisi tuna mguso wa Mbinguni, huko juu, ambao hutwambia ni Kweli. Basi tunasonga mbele kumsai huyo Ibilisi. Watu wetu wako shidani, kama tu Lutu alivyokuwa, katika lile somo asubuhi ya leo, naye Ibrahimu akaenda kumfuatilia.

¹⁹⁸ Shetani, tunakufuatilia, asubuhi ya leo. Maskini dada yetu aliyeachwa peke yake ana shida, nasi tunakufuatilia. Kwa mafuta ya kupaka, na kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa Neno la Kiungu la Mungu, na Injili, tunaenda kumwekea mikono, katika Jina la Yesu Kristo. Nasi tunakutoa kwake. Yesu alisema, “Enendeni,” wala haliwezi kushindwa; kasema, “Katika Jina Langu watatoa pepo.” Nawe ni pepo. Katika kutii amri Yake, tunakutoa kutoka kwake huyu, maskini... tunamwombea sasa, anayeonekana kama kwamba ameachwa peke yake. Damu ya Yesu inamtakasa na dhambi zote. Leo amekuwa msafi na mtakatifu machoni pa Mungu, kwa kukiri dhambi zake, kwa kusafishwa kwa Injili. Tunautupilia mbali, huu wasiwasi. Loo, naam, ulikuwa unamwita, bali huwezi kumgusa. Tunaomba ile Damu iwe kati yake na huu. Wao wanasimama kama mpatanishi. Na sasa mwache msichana huyu. Hebu awe huru. Na tangu leo na kuendelea, na awe na furaha. Kwa ajili ya hao watoto wachanga wanaolala pale.

¹⁹⁹ Kuhusu, mume huyo, jalia naye aje na awe Mkristo. Jalia wote walio wake, na siku moja Utukufuni, ile duara kuu ya jamaa isivunjike kule ng’ambo. Jalia mama yake, baba yake, wote walio wake, kila mmoja, awe Kule. Ee Mungu, jalia jambo hili.

²⁰⁰ Jalia awe huru kutoka wakati huu. Tunamweka huru, kwa upendo mkamilifu, na kuuamrisha kwa njia ya Biblia; na mauti, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu Kristo; kwa Damu Yake na Roho Mtakatifu. Tunamleta Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁰¹ Vema, nenda sasa. Mambo yatarudia hali ya kawaida. Unajisikia mzima sasa? Huumwi sasa; unajisikia mzima sasa.

²⁰² [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]...ukiwa namna hii daima, lingekuwa ni jambo zuri. Hakika. Amina. Sasa imekwisha, dada. Hiyo inakufanya upate faraja? Sasa unaweza kuondoka hapa, uende zako, uwe Ora May tena, ila tu, Ora May mpya, msichana mwenye furaha katika Kristo. Yote na yaishe. Urudi hapa, kama mwaka mmoja kutoka sasa, Mungu akipenda; urudi, useme, “Ndugu Branham, unakumbuka ile asubuhi uliyoniombea pale juu madhabahuni? Huo ulikwisha.” Mungu akubariki. Bwana asifiwe.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

²⁰³ Baba yetu wa Mbinguni, katika kutii agizo la Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo, tunakupenda leo, kwa upendo msafi, upendo matakatifu, usioghoishiwa. Basi jalia wema Wako

na rehema ziwe juu ya kila mmoja na watu wote. Tunakushukuru kwa ajili ya wageni ndani ya lango letu. Nasi tunaomba ya kwamba utambariki kila mmoja.

²⁰⁴ Mbariki mchungaji wetu mpenzi, Ndugu yetu Neville, anayesimama pamoja nasi katika lijamu ya Injili; hakufungiwa nira pamoja na ulimwengu, bali kafungwa lijamu pamoja na Kristo; amefungulia lijamu yote ya Mungu, huku anavuta gari la Injili ya zamani, akiendelea, wamefungwa nira pamoja kama raia wenzetu na watumishi wa Mungu.

²⁰⁵ Wabariki mashemasi wote, wadhamini, mweka hazina, na kila mmoja anayehusika, washiriki wote, waumini wa kawaida, wageni. Mungu, kutakuweko na mkutano kule Indianapolis. Mungu, mimi sistahili kubarikiwa, bali naomba uwabariki watu, kupitia kuhubiriwa kwa Neno! Hapana shaka ila mamia watasimama.

²⁰⁶ Pia tunampaka mafuta bibi huyu, katika Jina la Yesu Kristo, ili kwamba umsaidie na kumwondolea shida Yake, tunapomwekea mikono, katika Jina la Yesu Kristo. Sasa, Baba wa Mbinguni, jalia ya kwamba rehema Yako imfikie, katika Jina la Kristo.

²⁰⁷ Sasa huku tumeinamisha vichwa vyetu, sijui kama kuna mtu ye yote hapa ambaye ange—angekuja madhabahuni, angetaka kuja na kupiga magoti tuombe, ambaye amemkubali Kristo, ama unajisikia kana kwamba ungetaka kuomba kidogo baada ya huko kuzuriwa na Roho Mtakatifu. Hivi hamjisikii vizuri sana juu ya jambo hilo? Hamjisikii vizuri?

Njoo hapa, Ndugu Neville.

²⁰⁸ Ni wangapi wangeinua tu mkono wako, useme, “Ningetaka kuja madhabahuni kwa maombi mafupi tu.” Tafadhali inua mkono wako, useme, “Ningetaka kujitakasa, kidogo.” Loo, Mungu akubariki. Vema.

²⁰⁹ Sasa, mnaona, Ndugu yetu Neville, nafikiri, nimemwona katika mienendo yake yote, amekuwa mtu halisi. Ninamwona akiwa vile vile kila siku. Ama vita vinaendelea vizuri ama vinaendelea vibaya, Ndugu Neville habadiliki. Ninamshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hilo. Ndugu Neville asingeweza kufanya jambo hilo yeye mwenyewe; inahitaji Mungu kufanya jambo hilo. Nami ninafurahi ya kwamba kundi hili la kondoo lina mchungaji kama Ndugu Neville. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atamsaidia na kumbariki. Ninampenda. Pia nawapenda watu wake. Na tunawapenda ninyi nyote, na tunaomba ya kwamba Mungu atawabariki.

²¹⁰ Lakini sasa tunapoinamisha vichwa vyetu tena, nitaomba ya kwamba wale wangetaka kuombewa, na mnataka kupiga magoti na kujitakasa wenyewe, mngekuja kwa unyenyekevu madhabahuni.

²¹¹ Sasa, Ndugu Neville, waombee, tafadhali. Ninataka ninyi mwe ndani ya jambo hili. Kila mtu akiomba.

[Ndugu Neville anaanza kuomba—Mh.]

Tafadhalini njoni madhaba- . . .



UKAMILIFU SWA56-0610
(Perfection)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Juni 10, 1956, katika Maskani ya Branham, Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1996 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1996 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org